SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




UKURASA 3

**WAFUASI** wa CHADEMA jela kuharibu mali uchaguzi 2020




UKURASA 11

# Nipashe

Jumatatu Februari 21, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580863

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Madeni ya NSSF na NHIF yashtua

UKURASA 2



Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka

UKURASA WA 5

## SERIKALI ILIVYOPANIA KUBORESHA TIPPER KUHIFADHI MAFUTA

WAZIRI wa Nishati na Madini, January Makamba, amesema serikali imesaini mkataba na kampuni kubwa mbili kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kuingiza mafuta ikiwamo kiwanda cha kuhifadhia mafuta cha TIPPER kilichoko Kigamboni...

UKURASA WA 4

## WATUMISHI TARIME WASIMAMISHWA

MKUU wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi amewaondoa watumishi watano wa Halmashauri ya Tarime Vijijini ili kupisha tuhuma...

UKURASA WA 4

## MAZIKO YA MWELE KIJIJINI MVUMI LEO



MAZIKO ya Mwili wa Dk.Mwele Malecela ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Magonjwa yasiyopewa kipaumbele wa Shirika la Afya Duniani (WHO), yatafanyika leo Kijiji cha Mvumi wilayani Chamwino...

# Uwanja wa Ndege Dar kuboreshwa

UKURASA 2




## Majaliwa aiongezea kamati yake siku saba

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA QUEENS MECHI 11, MABAO 58, OPAH TISHIO UK.23 | MAONI, KATUNI UK.6



Mwendesha pikipiki akijaribu kunyanyua kiroba cha mkaa baada ya kudondoka na pikipiki kutokana na kufunga viroba vingi juzi, Mkuranga mkoani Pwani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madeni ya NSSF, NHIF yashtusha

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kuweka mkakati madhubuti wa kulipa madeni kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, huku likipongeza kupungua kwa deni la Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, aliwasilisha hoja hiyo bungeni jijini Dodoma mwishoni mwa wiki aliposoma taarifa ya mwaka 2020/21.

Alisema walibaini kuwapo kwa madeni ya mifuko kwa serikali na taasisi zake kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii nchini.

Kaboyoka alisema kuwa hadi Juni 30, 2020 deni la serikali lilikuwa Sh. trilioni 1.174, kwa kuanzia takwimu za mwaka 2007.

Mwenyekiti huyo alisema Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unaidai serikali zaidi ya Sh. bilioni 209.7.

"Madeni haya pamoja na kupunguza ufanisi wa mifuko husika, pia yanaharibu taarifa za mizania ya fedha kinyume cha Kanuni za Kimataifa za Uandaaji wa Hesabu," alitahadharisha. Kaboyoka alibainisha kwamba madeni hayo yamesababisha mifuko kushindwa kutimiza majukumu yake kisheria kwa ufanisi na kwa wakati.

Alisema deni la PSSSF lililohakikiwa ni Sh. bilioni 731 na walibaini kuwa hadi Juni 30, 2021 serikali ililipa Sh. bilioni 500, mwaka huu ikitoa hati fungani maalumu isiyo taslimu yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 1.176. "Bunge linapendekeza kwamba serikali iendelee na hatua za kulipa madeni husika kwa kutumia njia mbalimbali kama ilivyoanza katika mfuko wa PSSSF. Hatua hizi za serikali ziendelee katika mifuko ya NSSF na NHIF," Kaboyoka alihitimisha.

# Maboresho Uwanja JK Nyerere yaiva

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema akiwa katika ziara yake ya kikazi katika nchi za Ufaransa na Ubelgiji amesaini mikataba na kampuni ya ujenzi ili kuja kuboresha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) namba mbili (Terminal II).

Rais aliyesema hayo jana uwanjani hapo baada ya kwasili kutoka nchi za Ufaransa na Ubelgiji alipokwenda kwenye ziara rasmi ya kikazi.

Alisema hivi karibuni kampuni ya ujenzi ya Ufaransa itakuja kufanya marekebisho kwenye uwanja huo ambao miundombinu yake imechakaa.

"Terminal II ilijengwa na Wafaransa, imeshachakaa, tumekubaliana wanakuja kuifanyia ukarabati na walivyosema itaushinda Terminal III, kwa hiyo mkataba tayari, kampuni tayari tumesaini mkataba na karibuni watakuja na wataanza," alisema Rais Samia.

Rais Samia alisema pia alipokuwa huko alisaini mkataba wenye lengo la kufungua njia za uwekezaji ili kuwapa fursa za maendeleo machinga wa nchini.

"Machinga oyee, mpo wananguu, haya tumevuna kidogo kwa ajili yenu pia, tukiwa nchi zote mbili tulifanya mazungumzo na wafanyabiashara, tulifanya mazungumzo na Wafaransa, tukafanya mazungumzo na wafanyabiashara wa Ubelgiji, alisema na kuongeza:

"Tulitiliana saini mikataba kadhaa na hivi karibuni tunategemea kupokea ujumbe kutoka kwa wafanyabiashara kutoka Ufaransa na Ubelgiji pia waje kuona wapi wanaweza kuwekeza."

Alisema lengo la kuleta wawekezaji ni kuwapa nafasi wawekeze ili serikali itumie fedha zake katika masuala mengine ya maendeleo ambayo sekta binafsi haiwezi kuwekeza ili nchi isonge mbele.

Rais alisema pia akiwa nchini Ufaransa alifanikiwa kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza barabara za mwendo kasi na kilimo.

"Tukiwa Ufaransa kama mkuu wa mkoa alivyosema kuna vipesapesa tumevipata vya njia zetu za mwendo kasi na tumepata pesa kwa ajili ya shughuli za kilimo," alisema.

Alisema pia alifanya majadiliano kuhusu kujenga barabara za kupita magari ya kutumia umeme hivyo baada ya miaka mitano au sita ijayo Tanzania inaweza kuwa na hiyo teknolojia.

"Lakini kwenye mwendo kasi tulifanya mazungumzo kidogo wakaniuliza kwani haiwezekani Dar es Salaam au Dodoma kukawa na mabasi mbali na haya ya mwendokasi, njia ile tukaigeuza yakawa haya basi ya kwenda kwa umeme wanaita 'matrum' nadhani, hivyo baada ya miaka mitano, sita ijayo tunaweza kufika huko," alisema.

Vilevile akiwa nchini Ubelgiji Rais alisema licha ya kuhudhuria mkutano wa Umoja wa Afrika na Ulaya, alifanya mazungumzo na Serikali ya Ubelgiji ya kuwekeana mkataba wa mafunzo ili kuongeza nafasi za wanafunzi watakaokwenda kusoma nchini humo.

Rais alisema pia alitia saini mikataba yenye lengo la kuamua miradi iliyokwama kati ya hiyo miradi, mmoja umeshawekewa fedha na utekelezaji wake utaanza baada ya muda mfupi.

"Kama mnavyojua hapa katikati tulichokozana kidogo na Umoja wa Ulaya, uhusiano ukatetereka miradi ikakwama, tulikuwa na mradi wa kujenga airport nadhani za Kigoma, Shinyanga na Pemba, lakini mradi wa green cities, lakini tumeshakwamua, mradi mmoja umeshatiliwa fedha na hivi punde, kazi zitaendelea," alisema.

Vilevile alifanikiwa kupata kiasi cha Euro milioni 450 kutoka Euro bilioni 55, fedha za uwezeshaji kwa nchi za Kusini mwa Kangwa la Sahara Afrika kutokana na athari za UVIKO-19, fedha zitakazotumia kwa miradi ya miaka mitatu.

"Kwa hiyo tumejadili, tumeafikiana, tumefikia pahali, mikutano hii bado inaendelea hatujafikia maazimio ya mwisho, kutakuwa na mikutano mingine ili kujadili tufanyeje kwa dunia nzima," alisema Rais.

## Majaliwa aiongezea kamati yake siku 7

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiongeza siku saba kamati maalum iliyopewa jukumu la kuchunguza mauaji yaliyofanyika mkoani Mtwara na wilayani Kilindi mkoani Tanga.

Taarifa iliyotolewa jana na Ofisi ya Waziri Mkuu ilieleza kuwa; "Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ameridhia kuongeza muda wa siku saba kwa kamati maalum iliyopewa jukumu la kuchunguza mauaji yaliyofanyika Mtwara na Kilindi, Tanga. Kamati hiyo iliyoanza kazi Februari 4, mwaka huu, ilipaswa kukamilisha ripoti yake ndani ya siku 14, zilizoishia Februari 17. Lakini kutokana na ukubwa wa kazi na mahitaji ya kujiridhisha na baadhi ya masuala, kamati imeomba kuongezewa siku saba kuanzia Februari 17 hadi Februari 23.

Ilieleza kuwa; "Kamati hiyo iliundwa na Waziri Mkuu ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan alilolitoa Februari 4, mjini Magu, Mwanza akiwa njiani kuelekea Musoma, mkoani Mara kwenye maadhimisho ya miaka 45 ya CCM".

Taarifa hiyo pia ilieleza; "Aidha, Waziri Mkuu anatoa wito kwa mamlaka husika kuendelea kutoa ushirikiano kwa kamati ili iweze kuikamilisha kazi hiyo kwa wakati na ufanisi."

Februari 4, mwaka huu Rais Samia akiwa wilayani Magu akielekea katika sherehe za maadhimisho ya miaka 45 ya CCM mkoani Mara alimwagiza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuunda kamati huru kuchunguza tuhuma za mauaji mkoani Mtwara yanayodaiwa kufanywa na askari polisi.

Rais Samia alikosoa Jeshi la Polisi kuunda kamati ya kujichunguza wenyewe baada ya tukio hilo.

Rais Samia alisema; "Kuna mauaji yametokea Mtwara na kwa taarifa zilizoko polisi ndio lililofanya mauaji. Taarifa niliyonayo ni kwamba polisi wameunda kamati ya kufanya uchunguzi halafu walete taarifa."

"Haiwezekani jeshi lifanye mauaji halafu jeshi lichunguze lenyewe," amesema Rais Samia nakuongeza.

Kutokana na hali hiyo, Rais Samia alimwagiza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuunda kamati huru kuchunguza tuhuma za mauaji mkoani Mtwara yanayodaiwa kufanywa na askari polisi.

Baada ya agizo hilo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliunda kamati maalumu ya watu tisa ya kuchunguza mauaji yaliyofanywa Mtwara na Kilindi, Tanga.

Kamati hiyo ina maofisa wenye dhamana kutoka mamlaka tofauti za serikali ikiwamo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Rais, TAKUKURU, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu.

## HABARI KITAIFA

# Wanne CHADEMA jela miaka nane

**Na Said Hamdani**, LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi, imewahukumu wanachama wanne kati ya sita wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutumikia kifungo cha miaka nane kila mmoja, baada ya kupatikana na hatia ya makosa mbalimbali yakiwamo kuharibu mali zenye thamani ya Sh. milioni 22.2.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi, Consolata Singano, baada ya kuridhishwa pasipo na shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Waliohukumiwa ni aliyekuwa Diwani wa Kata ya Majengo, Rajabu Hassani Mfaume (45), Dadi Shayo (46), Hamisi Abdallah Seif Maleje (46) na Moshi Hamisi Mbelenje (26) wakazi wa Kata ya Majengo katika Halmashauri ya Mtama.

Kabla ya Hakimu Singano kutoa hukumu katika kesi namba 07/2020, washtakiwa walipewa nafasi ya kujitetea, ambapo kila mmoja kwa wakati wake aliomba aonewe huruma kwa madai ana familia inayomtegemea.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, aliulizwa na Hakimu Singano, kama anazo kumbukumbu za makosa ya zamani kwa washtakiwa na kujibu hana, huku akiomba mahakama kuwapa adhabu kali iwe funzo kwao na wengine wenye tabia za aina hiyo.

Mramba alidai kitendo cha kuharibu mali za umma si cha kiungwana, hakistahili kufumbiwa macho hivyo adhabu kali za kisheria zinahitajika kukomesha tabia ya aina hiyo.

Hakimu Singano akitoa hukumu kupitia vifungu mbalimbali vya kosa la kwanza kuharibu mali kila mmoja alimhukumu kutumikia kifungo cha miaka mitano jela, la pili kuisababishia hasara taasisi ya umma kulipa faini ya Sh. milioni moja kila mmoja au kwenda jela miaka mitano.

Kosa la tatu na la nne kuharibu mali za watu binafsi aliwataka kulipa faini ya Sh. 500,000, wakati kosa la tano hadi la sita kujeruhi na kusababisha maumivu kwa watu wengine aliwahukumu kifungo cha miaka mitatu kila mmoja, kwa vile adhabu zinaenda kwa pamoja, watatumikia kifungo cha miaka mitano.

Mahakama hiyo pia imewaachia huru washtakiwa wawili, Fatuma Ibrahimu Kumwalu (45) na Fatuma Raphael Protas (45) wakazi wa Kata ya Majengo, Halmashauri ya Mtama, baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha makosa yaliyokuwa yanawakabili.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na Mwanasheria wa Serikali, Mramba kuwa Oktoba 28, 2020, katika Halmashauri ya Mtama siku ya uchaguzi mkuu, washtakiwa wakitambua wanachofanya ni makosa waliharibu kwa kuchoma moto Ofisi ya Serikali ya Kata Majengo na kusababisha hasara ya Sh. milioni 20.7.

Mramba alidai licha ya ofisi ya kata pia walichoma moto pikipiki moja aina ya Snoley 110 yenye usajili namba MC 600 CCG yenye thamani ya Sh. milioni 1.6 mali ya Arafa Shaha Saidi na kufanya jumla ya Sh. milioni 22.3.

Pia washtakiwa hao walidaiwa kuwajeruhi kwa kuwashambulia kwa mawe na fimbo maeneo mbalimbali ya miili yao watu watatu, akiwamo askari Polisi WP 7657 Ester Kalaminyo, Hamza Hassani Zamea na Haifu Hamisi Abdallah.

# Mtambo kuokoa bil. 5/-

**Na Beatrice Shayo**

MTAMBO mpya utakaofungwa Juni mwaka huu, kwa ajili ya kubaini mwenye ugonjwa wa saratani mapema na tiba kemia itasaidia serikali kuokoa Sh. bilioni 5 zilizokuwa zinatumika kupeleka wagonjwa nje ya nchi kufanya vipimo vya saratani.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, wakati akijibu hoja za wabunge wa kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii walipofanya ziara ya kutembelea mradi huo unaojengwa katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI).

Alisema baada ya kukamilika kwa mradi huo Juni mwaka huu fursa iliyoko ni kuwatibu wagonjwa ambao walikuwa wanawapeleka nje ya nchi kufanya kipimo hicho na kutumia Sh. bilioni 5 kwa kila mwaka.

"Sasa tunakwenda kuokoa hii Sh. bilioni 5 ambayo ilikuwa inatumika huko nje ya nchi na pia tutauza mionzi kwa nchi nyingine ambapo za Kusini mwa Jangwa la Sahara na kwa nchi zinazotuzunguka zitakuja kununua miozi hapa nchini," alisema.

Alisema fedha hizo zitatumika kufanya matibabu kwa mwananchi mnyonge ambaye anatabiwa bila gharama.


**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**ARUSHA-ARUSHA**
**MAOMBI NA. 217 YA 2019**
**CREDO KIFUKWE.....MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**JUMA MGALA NYANGE.........MJIBU MAOMBI WA 1**
**YUSUFU ELPHAS MANGA....MJIBU MAOMBI WA 2**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA : JUMA MGALA NYANGE NA**
**YUSUFU ALPHAS MANGA...... POPOTE ULIPO**

**CREDO KIFUKWE**, amefungua shauri hili mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Arusha . Shauri husika limepangwa kutajwa mbele ya Mh.G.Kagaruki, Mwenyekiti tarehe 21/03/2021 saa tano kamili Asubuhi.
Hivyo basi,unatakiwa kuhudhuria siku hiyo wewe au wakili wako au mtu yeyote utakayempa maelekezo juu ya shauri hili.
Endapo hutatekeleza haya,shauri hili litasikilizwa upande moja na Hukumu kutolewa dhidi yako pasipo wewe kusikilizwa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri /Muhuri wa baraza hili leo tarehe 01 mwezi Februari,mwaka 2022.

**MWENYEKITI**



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**FORTUNATA APOLINARY MACHTIN**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 403 AEA yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba 0754847264
**DSM/PHQ/ RB/502412/2022**



**MISSING PERSON**

**NAME:** ELISHA O. ODERO ALIAS ELISHAMA OYIGO ALIAS ISHMAEL OIGO
**DATE OF BIRTH:** 1937
COMPLEXION: Tall & light skinned
**ORIGINAL HOME:** Mbihi Village Maragoli within Larger Kakamega, now Vihiga County, KENYA.
**PARENTS:** Reuben Oyigo Otiende (Reuben Odero Otiende) (late); and Loice Kalwara (late).
**SIBLINGS:** Rose Jendeka Nerea Mukilima; Erica Mmbone; Joshua Emboywa Otiende; and Catherine Jamodza.
**PROBABLE DAUGHTER:** JUDITH OTIENDE, from Tanzania.
**LAST KNOWN RESIDENCE:** Bamba Primary School in Tanga, Tanzania.
**RELIGION:** Christian (Salvation Army) or Islam.

**If you have any information that may lead us to him or to Judith Otiende, contact us through:**

**Contacts: +254712609333—His nephew: Ibrahim Otiende (Facebook: Ibrahim Emali Twitter: @Ibrahim_Emali) +254728998634—His Brother, Joshua Otiende +254724353735/+254782206035—His sister, Catherine Jamodz, Email: iemmally@rocketmail.com**

**DATED AT NAIROBI KENYA, 17 th FEBRUARY 2022**


## THE CONFEDERATION OF TANZANIA INDUSTRIES

## PRESS RELEASE

### Cement Manufacturers not Responsible for shortages reported

**Dar es Salaam, February 21, 2022.**

The Confederation of Tanzanian Industries (CTI) would like to comment on the media reports in the past months regarding the rising prices and availability of cement in the country.

Recently, it has been widely reported that the country is facing cement shortages and higher prices, and further linking the price increases and shortages to manufacturers.

Cement manufactures, most of whom being members of CTI, wish to announce that the status indicated by the media differs from the reality on the ground.

It is worth noting that at the meeting which was held on **31st January 2022** between cement manufacturers and the Minister of Industry, Investment and Trade (MIIT), **Hon. Dr. Ashatu Kijaji (MP),** cement manufacturers clearly indicated that cement is sold mostly by manufacturers at ex-factory prices which have not been increased in recent years.

Cement manufacturers further stated that the ex-factory prices have remained unchanged despite the increase in the cost of production resulting from the hike in the cost of fuel, transportation, and the inflationary spiral, among other things. It should also be noted that the cement industry is a capital-intensive venture that requires continuous investment and substantial maintenance costs to operate efficiently and remain competitive.

Most of the cement volume in the country is sold at an ex-factory price but transport cost has a significant impact on the landed price of the end product and fule prices have increased worldwide. Despite the fuel prices increasing by 45% over the last 18 months, the wholesale price of cement has remained stable in the main consumption centres.

Tanzania average cement manufacturing capacity utilization is around 60%, which means the supply is far above the country's total demand. With the country's new production capacities following the entrance of new manufacturers, any sudden demand spikes should be easily fulfilled. Furthermore, despite the increase in cement production capacity, cement manufacturers have been observing an increase in the influx of foreign cement from the neighbouring countries. CTI believes that such an influx in imports do jeopardize the future development of the cement industry in our country due to their competitive advantages in terms of logistics, port efficiencies and charges, energy and other infrastructures.

In view of the above facts, Cement manufacturers would like to inform cement consumers and the public of the availability of surplus cement in the country and further urge the media to carry out a thorough investigation on the shortages and prices of cement as and when such reports arise. Cement manufactures wish to offer their full cooperation on the matter. They will readily provide you with the necessary information on the stock position of the various producers and whole sales as and when required.

**By the CTI Secretariat**

216714401




Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa (watatu kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 36.6 ikiwa ni msaada kwa Mwenyekiti na Mwasisi wa Taasisi ya Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mama Mariam Mwinyi (wa nne kushoto), inayolenga kusaidia na kuboresha maisha ya watoto, vijana na wanawake wa Zanzibar katika hafla ya uzinduzi wa taasisi hiyo, iliyofanyika viwanja vya Mao, Unguja, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hapi asimamisha wa 5 Tarime kwa tuhuma

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKUU wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi, amewaondoa watumishi watano wa Halmashauri ya Tarime Vijijini ili kupisha tuhuma zinazowakabili.

Maofisa hao ni Ofisa Biashara, Mbuke Majula, Ofisa Ugani, Idd Baruna, Ofisa Uhasibu, Daniel Magwena, Mwanasheria wa Halmashauri, Alex Ifunya na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sirari.

Hapi alitangaza uamuzi huo wakati wa mkutano uliofanyika katika Mji wa Sirari wilayani Tarime mwishoni mwa wiki akiongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa.

Hapi alisema; "Baadhi ya watumishi wasio waadilifu katika halmashauri za Mkoa wa Mara wamehusika kwa namna moja ama nyingine kukwamisha shughuli za maendeleo ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka na fedha za umma."

Aliongeza: "Kuna Sh. milioni 500 ziliietwa na serikali tangu mwaka jana ili ziende katika ujenzi wa Kituo cha Afya Mtana Kata ya Manga, lakini zimekaa katika akaunti kwa zaidi ya miezi mitano bila kutumika na kukwamisha mradi huo."

Alisema: "Kuna Sh. milioni 140 zilizotolewa na Shirika la Hifadhi ya Taifa kwa ajili ya kununua gari lenye mashine ya kuchimba visima virefu katika hamashauri hiyo fedha hizo zimekwamishwa kwa zaidi ya miezi nane bila kununua lori hilo na mashine hiyo ya kuchimba visima."

Hapi alisema fedha nyingi zimekuwa zikiingia mifukoni mwa watu bila kufuata utaratibu wa kukusanya mapato ya halmashauri.

Pia alisema kumekuwa na madai ya madeni kwa halmashauri kesi karibu zote haishindi bali inashindwa.

"Inaonekana kuna mizengwe inafanywa kati ya wadai na wadaiwa na kusababisha halmashauri kushindwa kesi, namwondoa Mwanasheria wa Halmashauri, Alex Ifunya, katika halmashauri hii," alisema Hapi.

Hivyo, Hapi aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Polisi kuwachunguza watumishi hao.

# Wabunge sasa wautaka Muswada Sheria ya Polisi

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wamesema ipo haja kwa serikali kupeleka bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria iliyoanzisha Jeshi la Polisi, irekebishwe iendane na hali ya sasa na kuongeza uwajibikaji.

Wabunge hao walitoa mapendekezo hayo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma, wakati wa semina kwa wawakilishi hao wa wananchi vinara wa haki za binadamu iliyoandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Mbunge wa Liwale, Zuberi Kuchauka, alisema ni lazima kutenganisha mamlaka ndani ya Polisi, ili kudhibiti na kurejesha imani kwa raia, kwa kuwa sasa siyo kimbilio tena.

"Mtu akipata madhara anakimbilia polisi, lakini hao hao wanamgeuka na kumkamata kisha wanampa kesi. Tuunde Jeshi la Polisi, kuliacha lilivyo ni hatari wananchi wanaumia na hawana pa kukimbilia," alisema.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, alisema imefika mahali wananchi hawawezi kudai haki yao zaidi wanaonekana wakorofi na wataunganishwa kwenye kesi.

"Mfano, leo hii mtu akiona mtu amekufa kwenye korongo fulani anaogopa kutoa taarifa maana atakamatwa wa kwanza, sasa nani atawapa taarifa, wao siyo Mungu, tulikuwa na polisi jamii, lakini haijasaidia," alisema.

Mtaturu alisema kwa sasa hakuna namna ya kuwapo kubadilisha sheria na kutenganisha mamlaka ili kuwa na jeshi la kisasa na lenye kuwajibika.

"Tumeona hivi karibuni walitangaza nafasi za kazi wakasema wanataka wenye elimu fulani maana hawatakiwi kupanda wawe maofisa, sasa hii siyo sawa," alisema.

Alisema haki za wengi zinaminywa kwasababu ya baadhi ya polisi wenye nia ovu hata kiwango cha elimu na kwamba sheria ni hitaji la jamii, inapofikia mahali ikaonekana upo umuhimu ni vyema kusikiliza.

Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, alisema Sheria ya Jeshi la Polisi imepitwa na wakati na ndiyo maana mara nyingi bungeni amependekeza kuanzishwa kwa sera ya ufuatiliaji na upimaji.

"Lazima majukumu ya IGP na Mkurugenzi wa Upelelezi Nchini (DCI) yatenganishwe , turekebishe sheria iendane na mahitaji halisi ya sasa... ni aibu sasa kwa miaka 60 tunatumia sheria ya kikoloni licha ya kwamba tumesaini mikataba mbalimbali ya haki za binadamu," alisema.

Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka, alisema mfumo wa Jeshi la Polisi ni wa tangu ukoloni ambao ni kandamizi kwa kuwa wao kukamata, kupiga au mabavu ili kupata ukweli ndiyo msingi badala ya kutumia akili.

"Tunapofumua jeshi hili kuwe na polisi, wapelelezi na waendesha mashtaka na siyo huyo huyo akamate, apelelezi, ashtaki, mahakamani waendesha mashataka wakiharibu kesi basi hata jaji au hakimu hawezi kufanya lolote, wakitaka kukukomoa wanaharibu tu kesi yako katika hatua za awali," alisema.

Awali, Ofisa Uragibishi wa LHRC, Willium Maduhu, alisema wamebaini wananchi wengi haki zao zinaporwa na polisi, mara nyingi wamewashauri waende kushtaki kwa wakubwa wao, lakini wameishia kusumbuliwa na wapo wenye rundo la barua za malalamiko na hazijafanyiwa kazi.

# Maziko ya Mwele leo, Mpango ammiminia sifa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAZIKO ya mwili wa Dk. Mwele Malecela ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Magonjwa yasiyopewa Kipaumbele wa Shirika la Afya Duniani (WHO), yatafanyika leo Kijiji cha Mvumi wilayani Chamwino.

Dk. Mwele (58) alifariki dunia Februari 10 Mjini Geneva, Uswisi wakati akiendelea na matibabu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana kwa waombolezaji nyumbani kwa baba wa marehemu, ibada ya maziko itaanza saa tatu asubuhi leo katika Kanisa la Kuu la Roho Mtakatifu la Anglikana Dayosisi ya Cetral Tanganyika na itaongozwa na Dk. Dickson Chilongani, huku viongozi mbalimbali wa serikali na wa taasisi za nje ya nchi wanatarajiwa kushiriki.

Baada ya ibada hiyo sehemu ya kwanza msafara utaelekea Kijiji cha Mvumi kwa ajili ya kupumzishwa kwenye nyumba yake ya milele.

Katika hatua nyingine, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango na mkewe, Mbonimpaye Mpango, jana walifika nyumbani kwa Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, jijini hapo kwa ajili ya kutoa pole kutokana na kifo cha mtoto wake.

Akitoa neno la faraja kwa familia na waombolezaji mbalimbali waliojitokeza nyumbani hapo, Makamu wa Rais, alimtaja Dk. Mwele kama shujaa aliyejitoa kupigania afya za wananchi wengine kupitia tafiti mbalimbali alizokuwa akizifanya zenye lengo la kusaidia jamii kupambana na magonjwa mbalimbali.

Alisema Dk. Mwele alifanya kazi iliyo njema na kuonekana katika jamii ndani na nje ya nchi.

Aidha, alisema katika kipindi cha uhai wake Dk. Mwele aliinua jina la Tanzania kwa kuaminiwa kufanya kazi katika taasisi kubwa ya afya duniani.

"Uwezo wa Dk. Mwele katika kazi pia uliinua wanawake nchini, hivyo hapana budi kumshukuru Mungu kwa zawadi hiyo pamoja kumwombea apokee ili apumzike kwa amani," alisema.

Dk. Mwele kabla ya kuteuliwa kushika wadhifa huo alikuwa Mkurugenzi wa Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa Afrika (Espen), WHO Kanda ya Afrika.

Pia Dk. Mwele aliwahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kabla ya kuvuliwa wadhifa na Hayati Rais John Magufuli Desemba 17, mwaka 2016.

Mwaka 2015, Dk. Mwele alikuwa mmoja wa watia nia ya kugombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

# Serikali sasa kuiboresha TIPPER kuhifadhi mafuta

**Na Jenifer Gilla**



WAZIRI wa Nishati na Madini, January Makamba (pichani), amesema kuwa serikali imesaini mkataba na kampuni kubwa mbili kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kuingiza mafuta ikiwamo kiwanda cha kuhifadhia mafuta cha TIPPER kilichoko Kigamboni Dar es Salaam.

Aliyasema hayo bungeni wiki iliyopita alipokuwa akijibu hoja na ripoti iliyowasilishwa na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini.

"Sasa nataka niwape habari njema kwamba kabla ya mwisho wa mwezi huu tutasaini MOU na kampuni kubwa mbili ya kufumua miundombinu yote ya uingizaji na ushushaji wa mafuta," alisema Makamba na kuongeza:

"Tunaenda kuibadilisha TIPPER na kuweka uwekezaji mkubwa ambao utaongeza uwezo mara tatu...kwa hiyo tumeamua tutaweka mabomba makubwa zaidi, na sio ya dizeli peke yake, tutaboresha matangi, hiyo kazi itachukua kama miaka mitatu lakini itabadilisha kabisa mfumo mzima wa ushushaji mafuta nchini."

Alisema changamoto iliyo sasa ni kwamba mabomba yanayopitishia mafuta kutoka kwenye meli ni membamba na kusababisha upakuaji kuchukua muda mrefu hivyo moja ya mambo watakayoyafanya ni kuweka mabomba makubwa.

Alisema sekta ya mafuta kwa siku inachangia Sh. bilioni 5.1 kwenye shughuli za maendeleo na kwa mwaka ni trilioni 1, hivyo ni muhimu kutunza vizuri ili kuchangia katika maendeleo.

Makamba alibainisha hayo kutoa maelezo kufuatia ripoti iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Dustan Kitandula, aliishauri serikali kuanza kutumia ghala la kuhifadhi mafuta la TIPER ili kuondoa tatizo la meli kusubiri kwa muda mrefu kuingia bandarini na kupunguza gharama za ucheleweshaji wa meli.

Alisema njia hiyo inaweza kuanza kutumika kwa kipindi cha mpito wakati serikali ikijapanga kujenga sehemu moja ya kupokelea shehena ya mafuta.

Kitandula alisema kuongezeka kwa bei ya mafuta kunachangiwa na sababu mbalimbali ikiwamo kupanda bei ya mafuta katika soko la dunia, changamoto ya miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam na uwezo mdogo wa maghala ya kupokelea na kuhifadhi mafuta nchini

Pia ameshauri kujenga maghala makubwa ambayo yatahifadhi mafuta zaidi ya mita za ujazo milioni 1.25 ili kuifanya Tanzania kuwa 'hub' ya biashara ya mafuta kwa nchi zinazotuzunguka na kuagiza mafuta mengi zaidi wakati bei ya mafuta imeshuka katika soko la dunia," alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni Naibu Mkurugenzi wa TIPPER, Martin Mosha, alisema kuwa iwapo kiwanda hicho kitapewa nafasi inaweza kuchangia kufanya bei ya mafuta isipande mara kwa mara kwa kuhifadhi kiasi kikubwa cha mafuta kwa muda mrefu zaidi.

# Mbaroni tuhuma kuiba kichanga kituo cha afya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia mkazi wa Kata ya Lugunga wilayani Mbogwe mkoani Geita, Rehema Saidi (47) kwa tuhuma ya kuiba mtoto mchanga wa siku 20 katika Kituo cha Afya Lunguya kilichoko Halmashauri ya Msalala mkoani hapa.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga (ACP) Joseph Haule, amethibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo Februari 17, mwaka huu, akiwa na mtoto huyo baada ya kufanyika kwa upelelezi.

Alisema tukio hilo lilitokea Februari mosi, mwaka huu, majira ya saa 11 jioni kwenye Kituo cha Afya Lunguya.

Kamanda Haule alisema mtoto huyo ambaye ni wa kiume aliibiwa kitandani na kupatikana wilayani Mbogwe mkoani Geita akiwa mikononi mwa mtuhumiwa huyo.

Mama mzazi wa mtoto huyo, Betha Augustino (21), alivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi kwa kufanikisha kupatikana kwa mtoto wake.

"Ninafuraha kumpata mwanangu, naipongeza serikali hususani Jeshi la Polisi na vyombo vya habari kwa kuchapisha habari zilizosababisha mwanangu kupatikana kwani watu wengi wamenipigia simu baada ya kusoma taarifa hizo,"alisema Augustino.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Novelt Furaha aliomba serikali kuimarisha ulinzi katika vituo vya afya, zahanati na Hosptali ya Wilaya ili kudhibiti matukio ya wizi wa watoto hususani katika wodi za kujifungulia.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Msalala, Dk. Joseph Muyeye, alikili kutokea tukio la wizi katika kituo cha afya hicho na kwamba mtoto huyo amechunguzwa afya yake na kukutwa yupo vizuri.

Alisema aliyemuiba mtoto huyo alikuwa anamnywesha maziwa ya ng'ombe hivyo wamewashauri wazazi hao waendelee kumnywesha maziwa hayo bila kumbadilishia.

Alisema ili kuendelea kudhibiti vitendo vya aina hiyo wameweka madaftari maalum ya kusaini unapoingia na kutoka katika wodi zote zilizoko katika vituo vya afya.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA YA WALINZI WA USALAMA NA HUDUMA ZA MAPOKEZI KATIKA OFISI YA DAR ES SALAAM**
**REJEA NO. 0010007504**

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, linayaalika mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuonesha nia yao ya kutoa huduma za ulinzi na mapokezi kwenye mradi wa EACOP Ofisi ya Dar es Salaam. Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

- Kutoa huduma za ulinzi wa saa 24/7 kwa majengo ya ofisi.
- Kutoa huduma za mapokezi wakati wa saa za kazi – sharti awe anazungumza Kiingereza.
- Kutoa huduma za ufuatiliaji katika Chumba cha Udhibiti wa Usalama saa 24/7 - sharti awe anazungumza Kiingereza.
- Kutoa Msimamizi wa shughuli za Usalama aliye na bidii na mwaminifu.
- Kutoa huduma za taarifa za Kiusalama kwa Ukanda wa Afrika Mashariki, hasa Tanzania na Uganda.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi yakimbatanisha nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa ISO18788.
- Uthibitisho wa kuzingatia Kanuni za Kujitolea za Umoja wa Mataifa za Ulinzi na Haki za Binadamu (VPSHR).
- Uthibitisho kwamba taratibu za ajira zinaepuka kuajiri wafanyakazi wanaokiukaji haki za binadamu.
- Kuonesha uwezo wa kusimamia shughuli za usalama, kutoa mafunzo na kwamba anatekeleza sera thabiti ya Uwajibikaji kwa Jamii kwa mujibu wa kanuni za kazi za kitaifa.
- Sampuli ya vifaa vya mafunzo kwa walinzi, mtu wa mapokezi, mwendeshaji wa SCR, na msimamizi. *
- Sampuli ya uchunguzi wa Tukio, utaratibu wa kuripoti na fomu za vielelezo.
- Rejea ya huduma alizowahi kufanywa zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa uwezo wa kampuni kimtaji katika utoaji wa huduma.
- Uthibitisho wa leseni za Biashara na leseni zote za udhibiti au uidhinishaji unaohitajika ili kutoa huduma hizi.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha kuthibitisha kulipa kodi kwa mwaka uliopita.
- Wakati wa kuwasilisha maombi inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kanzidata ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa kutuma maombi haya.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa makampuni ya ndani.

  Kumbuka; vifaa vya mafunzo vinapaswa kuwa sampuli tu, uwasilishaji wa mwongozo kamili wa mafunzo HAUTAKIWI. Hata hivyo, ni muhimu kujumuisha muhtasari wa mtaala (syllabus) na maelezo ya ratiba ya mafunzo/ratiba ya urejeaji mafunzo.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00** alasiri saa za Afrika Mashariki (EAT), **4th March 2022 .** Kichwa cha habari cha Barua pepe kiwe ni **0010007504.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa taasisi za awali zenye vigezo baada ya taasisi hizo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza

216712101

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba mkifanya kweli hapa, robo fainali CAF itawahusu

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania katika michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba, jana usiku walishuka katika Uwanja wa Generali Seyni Kountche nchini Niger, kucheza mechi yao ya pili ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Union Sportive Gendarmerie Nationale, USGN.

Lakini mchezo huo dhidi ya USGN ukiwa wa kwanza kwa Simba ugenini baada ya kushinda mechi yake ya kwanza nyumbani kwa mabao 3-1 dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili ya Februari 13, mwaka huu.

Matokeo hayo yaliifanya Simba na RS Berkane ambayo ilishinda nyumbani kwa mabao 5-3 dhidi ya USGN, kukaa kileleni kila moja ikifikisha ponti tatu katika Kundi lao la D ambalo linatabiriwa kuwa gumu zaidi.

Ikumbukwe kuwa kwenye michuano hiyo kuna makundi manne kila moja likijumuisha timu nne na zitakazoshika nafasi ya kwanza na ya pili kutoka katika kila kundi, zitafuzu moja kwa moja hatua ya robo fainali.

Hivyo, ili kuwa na uhakika wa kufuzu kwanza ni timu kuhakikisha inashinda michezo yake ya nyumbani na angalau kuvuna pointi nne ugenini, kwa kushinda mechi moja na sare moja.

Kwa uzoefu tulionao katika kufuatilia michuano hiyo ambayo hufanyika kila msimu, ili timu kukamilisha mapema hesabu zake za kufuzu robo fainali ni kutofanya makosa katika mechi hizi tatu za mzunguko wa kwanza.

Tayari Simba imeanza vema mechi yake ya kwanza nyumbani kwa ushindi na ratiba imeangukia vizuri upande wao ambapo itacheza mechi mbili mfululizo ugenini kuanzia ya jana kabla ya kukamilishia ratiba hiyo nyumbani.

Baada ya mchezo wa jana usiku, Simba imesema itaweka kambi nchini Niger kabla ya kuifuata RS Berkane nchini Morocco kwa mechi yao ya tatu kukamilisha mzunguko wa kwanza wa hatua hiyo ya makundi.

Hivyo, kinachotakiwa kwa Simba ni kuhakikisha inapata matokeo chanya katika mechi hiyo ambayo tunatarajia ndio utakuwa mchezo mgumu zaidi kwao kuliko mingine yote ya kundi hilo.

Hata hivyo, tunaamini kwa uzoefu mkubwa Simba ilionao kwenye michuano ya kimataifa, haitaliangusha taifa na tukiwa wadau wakubwa wa michezo nchini, tunatarajia kuiona hatua ya robo fainali ya mashindano hayo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

Tunachotarajia kukiona ni Simba ikibeba vema jukumu hilo la kuipeperusha bendera ya Tanzania katika medani ya soka kimataifa na kuzipigania nafasi za kuingiza timu nne kwenye michuano ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF); mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho kwa msimu ujao.


Lengo letu ni kuona kila mwaka Tanzania inakuwa miongoni mwa mataifa 12 Afrika yanayoingiza timu nne katika michuano hiyo ya CAF na katika hilo hakuna njia ya mkato zaidi ya kila mpenda soka nchini kusimama kidete kuiombea Simba kufanya vizuri kwenye michuano hiyo kwa sasa.

Ikumbukwe tayari kuna nchi 11 zenye pointi nyingi za kuziwezesha kuingiza timu 12, ambazo kwa msimu huu pekee Tanzania haiwezi kuzipiku, na nafasi iliyobaki ni moja ambayo inawania pia na Libya yenye timu mbili katika michuano hiyo ya CAF, hivyo Simba ikishindwa kufuzu robo fainali na kuendelea ni wazi tutaipoteza nafasi hiyo.

Kikubwa kwa sasa ni kila mmoja kuiombea Simba kufanya vizuri na kusonga mbele hata ikiwezekana kufika hata nusu fainali ama fainali huku tukiziombea timu hizo za Libya kuaga mapema michuano hiyo, jambo ambalo tunaamini kilichobaki ni dua zetu tu kwani kwa suala la uwezo na uzoefu hatuna shaka na wawakilishi wetu hao, katika hilo hatuna budi kuitakia kila kheri kwa majukumu hayo mazito.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ufinyu mabao Ligi Kuu tatizo lipo hapa

Na Adam Fungamwango

**UKIACHANA** na Kombe la FA ambapo timu zinabugizwa mabao sita mpaka saba, bado idadi ya mabao kwenye mechi nyingi za Ligi Kuu haziridhishi.

Matokeo ya bao moja au mbili, ndiyo yametawala kwenye mechi nyingi za Ligi Kuu. Ni mara chache sana kuona timu ikipata ushindi wa mabao kuanzia matatu kwenda mbele msimu huu. Tuliona msimu uliopita, timu kama Simba ikipata ushindi wa mabao mengi kwenye mechi kadhaa za Ligi Kuu. Na haikuwa msimu uliopita tu, karibuni misimu minne, Simba ilikuwa timu ambayo ilikuwa ikipata ushindi wa mabao mengi kwenye baadhi ya mechi zake.

Ushindi mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu msimu huu, Simba iliupata Desemba 24, mwaka jana ilipoichakaza KMC mabao 4-1 katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, mkoani Tabora, na pia ilipoichapa Ruvu Shooting 3-1 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Hata Yanga nao, pamoja na kwamba msimu huu iko vizuri kuliko misimu mingine iliyopita, lakini bado haipati ushindi ambao wanachama na mashabiki wao inautarajia kutokana na ubora wa michuano hiyo. Mpaka sasa ushindi mkubwa wa Yanga kwenye Ligi Kuu ni ule wa Desemba 31, mwaka jana, ilipochapa Dodoma Jiji mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, na unaokaribiana na huo ni ule wa Novemba 2, ikiibamiza Ruvu Shooting 3-1.

Angalau Azam, ambayo imepata ushindi wa mabao manne kwenye mechi mbili mpaka sasa, ilipoibamiza Ruvu Shooting mabao 4-1 Desemba 23, mwaka jana na 4-0 dhidi ya Prisons Januari 22, mwaka huu.Ukiacha timu hizo kubwa, matokeo ya timu zingine zikicheza zenyewe kwa zenyewe ndiyo hayaridhishi kabisa. Huwa kama si suluhu, sare ya bao 1-1, basi zitafungana 1-0, 2-1, ikizidi sana mabao 2-0.

Huwezi kukuta mechi kama ya msimu uliopita, ambapo JKT Tanzania iliichakaza Mwadui mabao 6-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Oktoba 28, 2020, au mechi zingine ambazo zilikuwa na idadi kubwa ya mabao.

Kwa sasa ni za kuhesabu, tena kwa timu kubwa, ambazo pia nazo ni kama nazo zimeanza kupungua, ingawa ligi haijamalizika. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha kuwa mzunguko wa pili ndiyo huwa mgumu zaidi kuliko wa kwanza.

Tatizo ni nini? Inawezekana ikawa ni viwanja, hasa vya mikoani havipo kwenye hali nzuri, hali inayosababisha wachezaji kuwa na kazi ngumu ya kuuweka mpira wavuni. Yupo mtu anaweza akahoji, mbona viwanja ni vibovu hata wakati timu zinashinda mabao mengi huko nyuma.

Ni kweli, lakini inavyoonekana kila muda unavyozidi kwenda viwanja hivyo navyo vinazidi kuwa vibovu zaidi. Na kwa sasa tumeona kuna baadhi ya mikoa mvua kubwa inanyesha, huku mechi zikiendelea, wachezaji wakipata tabu hata kupiga tu mpira, achilia mbali kukokota.

Tatizo la viwanja nalo linapunguza uhondo wa kuona mabao mengi yakifungwa kwenye Ligi Kuu. Pili ni kwamba msimu huu timu nyingi zimejizatiti. Wadhamini wa Ligi Kuu, wamewekeza pesa, ambazo zimefanya timu nyingi kulipa mishahara na posho za uhakika, hivyo wachezaji kujituma.

Kingine ni kupungua kwa timu za Ligi Kuu. Kwa sasa kuna timu 16 tu. Wachezaji wa timu nne zilizopunguzwa msimu miwili nyuma kulipokuwa na timu 20, tunawaona wameenda kuziongezea nguvu timu zilizobaki, hivyo kuwa imara.

Mwisho ni ukweli mchungu kwamba, kuna tatizo kubwa la ufungaji kwa wachezaji wengi wanaocheza Ligi Kuu. Ukiangalia zinapatikana nafasi nyingi, lakini wanashindwa kuweka mpira ndani ya wavu. Ni wachezaji wachache sana kwenye Ligi Kuu wenye uwezo wa kutumia nafasi chache zinazopatikana kufunga mabao.

## Walalamikia 'machangudoa' kufurika msimu wa mavuno

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAWAKE katika vijiji wilayani Shinyanga, wamelalamikia kitendo cha madadapoa maarufu 'machangudoa' kutoka mjini kwenda huko kipindi cha mavuno, kufanyabiashara ya kujiuza kwa kubadilishana na zao la mpunga. Walisema hali hiyo inasababisha familia zao kukosa chakula kwa kuwa wanaume wananunua madadapoa hao kwa kuwapa mpunga.

Wanawake hao kutoka vijiji vya Lyamidati na Lyabukande wilayani Shinyanga, walipaza sauti hizo juzi kwenye mafunzo ya kujengewa uwezo wa namna ya kupambana na matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, yaliyotolewa na Shirika la Agape.

Mmoja wa wanawake hao kutoka kijiji cha Lyamidati, Matha Malale, alisema kipindi cha masika familia zao zinakuwa na upendo, lakini msimu wa mavuno ukifika migogoro inaanza kuibuka.

"Matukio mengi ya ukatili wa kijinsia ambayo yapo huku vijijini ni wanaume kutelekeza familia huku chanzo chake kikubwa kikitajwa kuwa ni wimbi la madadapoa kutoka mjini ambao wanaokwenda vijijini kipindi cha mavuno kwa ajili ya kufanyabiashara ya ngono kwa kubadilishana na mazao," alisema.

"Chakula kinapoisha ndani ndipo mwanaume anaona aibu na hatimaye kuamua kutoweka kabisa nyumbani, na kuiacha familia yake ikihangaika kukabiliana na njaa," aliongeza. Naye Anastazia Karali kutoka Kijiji cha Lyabukande, alisema mwanaume anapotoa chakula kwa madadapoa, wakijaribu kuwazuia wanaambulia kipigo na hivyo kuamua kunyamaza, huku wakitafuta mbinu mbadala ya kuficha baadhi ya chakula ili siku wakitelekezwa wapate cha kuwapa watoto. Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Lyamidati wilayani Shinyanga, Irene Mchuma, alisema kipindi cha mavuno kesi nyingi za migogoro ya familia, ikiwamo vipigo kwa wanawake huongezeka.

Aidha, alisema baada ya mazao kuisha katika familia wanaume wengi hukimbia nyumbani na kwenda kusikojulikana kukwepa aibu.

Alisema baada ya kuona tatizo hilo linakuwa kubwa, waliamua kujadiliana na uongozi wa jeshi la jadi (Sungusungu), ili kudhibiti wimbi hilo la madadapoa kuvamia maeneo hayo ya vijijini kipindi cha mavuno.

Aliongeza kuwa licha ya kukabiliana na tatizo hilo, lakini bado madadapoa wanaingia katika vijiji na kufanya biashara za ngono kwa siri.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Shinyanga, Christopher Malengo, alisema tatizo hilo la madadapoa kuvamia maeneo ya vijijini ni kubwa.

Alisema madadapoa hao wanatoka mikoa ya Singida na Manyara na kwamba kabila la Wasukuma wanapenda wanawake weupe na hivyo kuwa rahisi kupata biashara.

Alisema madadapoa wanawapa wanaume hao masharti kwamba wakitaka kuona maumbile yao, wanatoa debe moja la mpunga na wakifanya tendo moja la ngono wanalazimika kulipa gunia moja la mpunga.

Alisema kwa wastani dadapoa mmoja anafikisha gunia 100, katika msimu mmoja anazokusanya kutoka kwa wanaume na kuzisafirisha kwenda kwao huku familia za wanaume zikibaki na njaa.

"Mwanaume akimaliza kabisa chakula ndani na akapagawa na huyo mwanamke kama ana mifugo anaanza kuiuza na mifugo ikiisha ndipo anaamua kuikimbia familia yake kwenda kuanza maisha upya huko atakapokwenda," alisema Malengo. Alisema mipango ambayo wanaifanya kwa sasa licha ya kuzuia madadapoa hao kwenda maeneo ya vijijini kipindi cha mavuno, pia wanatoa elimu ya kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, malezi bora ndani ya familia na namna ya kutumia mavuno vizuri kujikwamua kiuchumi na siyo kwenye anasa. Meneja miradi kutoka Shirika la Agape, Peter Amani, aliwataka wanaume wa maeneo hayo ya vijijini kuachana na mila kandamizi, ambazo zimekuwa chanzo cha migogoro na ukatili ndani ya familia kwa kumnyima sauti mwanamke, pamoja na kuwa na haki ya kusimamia mavuno ya mazao.

Baadhi ya wanaume wa maeneo hayo ya vijijini, walikiri kutumia mazao pamoja na mifugo katika masuala ya ngono na kwamba kinachowasumbua ni ulimbukeni wa kupenda wanawake wa mjini sababu ya unadhifu wao na kuwapa mapenzi mazuri.

## UVIKO-19 ilivyochochea kasi wenye kifafa kupata degedege

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA kipindi cha mlipuko wa virusi vya UVIKO -19, kasi ya wagonjwa wenye kifafa kilichodhibitiwa kupata degedege iliongezeka.

Hayo yalisemwa na Dk. Edward Kija, Daktari Bingwa wa Mfumo wa Fahamu na Ubongo kwa Watoto kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, alipokuwa akiongea na Nipashe ofisini kwake, akieleza changamoto wanazokumbana nazo katika kipindi hiki cha mlipuko wa UVIKO-19.

Alisema kwa kawaida mgonjwa wa kifafa anapokunywa dawa zake inavyotakiwa huwa hapati degedege labda kama akipata maradhi nyemelezi ikiwamo homa, mafua na maambukizi mengine ya bakteria.

"Sasa kipindi ambacho UVIKO-19 ulishamiri homa na mafua navyo vilisambaa na hii iliwapata hadi wagonjwa wetu tunaowahudumia wa kifafa hali iliyosababisha hata wale ambao ugonjwa wao tuliudhibiti wakawa wanapata degedege," alisema Dk. Kija.

Hata hivyo, alisema walifanikiwa kudhibiti ongezeko hilo kwa kuwapatia dawa za kutibu magonjwa hayo nyemelezi na kuwapatia elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

"Mara nyingi mgonjwa wa kifafa anayetumia dawa zake vizuri akipata degedege tunampima na kumpatia dawa za kisababishi cha ugonjwa huo, kwa wale waliokuwa na homa tuliwapa dawa na wa mafua kadhalika," alisema na kuongeza:

"Lakini tulikuwa tunawafundisha wazazi mbinu za kuwakinga watoto wao na ugonjwa wa corona ikiwamo kunawa mikono, kuepuka msongamano, na kukaa umbali wa mita moja, na hata wanaporudi kutoka kwenye mihangaiko kujisafisha kwanza kabla ya kuwahudumia watoto," alisema.

Njia nyingine alisema ni kuwapatia wagonjwa vidonge vya muda mrefu ili kuwapunguzia safari za kwenda kliniki mara mara na kukutana na mikusanyiko ya watu hali inayoongeza maambukizi ya UVIKO -19.

"Wagonjwa ambao kifafa chao tumekidhibiti na wapo katika hali salama tulikuwa tunawapa vidonge vya kutumia hadi miezi mitatu ili kuwaepusha na mikusanyiko isiyo na lazima," alisema.

Naye Latifa Iddi, mzazi wa mtoto mwenye tatizo la kifafa alikiri kuwa wakati UVIKO-19 unaingia mtoto wake alikuwa akipata mafua mara kwa mara hali iliyopelekea kupata degedege tofauti na hapo nyuma.

"Mwanangu alikuwa akipata mafua mara kwa mara, hali iliyoongeza kasi ya kupata degedege, yaani ilikuwa kila baada ya wiki anaumwa homa au mafua na kupata




Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, akivishwa skafu baada ya kuwasili kwenye maadhimisho ya kumbukumbu ya Siku ya Mwanzilishi wa Skauti Duniani, ambaye ni mgeni rasmi akimwakilisha Mkuu wa Mkoa, yaliyofanyika viwanja vya Sabasaba, mkoani Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## Chanjo UVIKO-19 yaanza kila baada ya ibada Kanisa Katoliki

**Na Sabato Kasika**

KANISA Katoliki Parokia ya Magomeni Dar es Salaam, limeweka utaratibu wa kuita watoa huduma ya chanjo ya UVIKO-19 ambao huwa wanachanja waumini kila baada ya ibada za Jumapili.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Parokia hiyo, Thomas Ngawaiya, ameliambia gazeti hili kuwa tangu chanjo izinduliwe mwishoni mwa Julai mwaka jana, huduma hiyo imeshatolewa mara tatu kanisani hapo.

Ngawaiya alisema, lengo la kufanya hivyo ni kutaka waumini wapate huduma hiyo karibu badala ya kuifuata umbali mrefu, ambapo wengine hushindwa kutokana na majukumu mbalimbali walionayo.

"Ni utaratibu ambao tumejiwekea ili wale wanaotaka kuchanjwa wapate huduma hiyo kwa urahisi bila kuifuata umbali mrefu, na inawezeakana wahudumu wa afya wakaja tena kutoa chanjo," alisema Ngawaiya.

Ngawaiya alisema, kanisa limejiwekea utaratibu huo baada ya serikali kuziomba taasisi za dini kuhamasisha waumini kupata chanjo, na kwamba parokia hiyo imepiga hatua hadi kusogeza chanjo kanisani.

"|Kwa hiyo sisi katika parokia yetu si kuhamasisha chanjo tu bali tumefanikiwa kuwaleta watoa huduma ya chanjo kuja kuchanja watu kanisani kwetu na huenda tukawaleta tena kutoa huduma hiyo," alisema.

Alisema, katika kupambana na ugonjwa huo, kanisa limeona litumie njia hiyo ya kuhamasisha waumini kwenda kwenye vituo vya kutolea chanjo, lakini kusogeza huduma hiyo kanisani.

"Tunajua kuwa suala la chanjo ni hiari, lakini hatuna budi kukumbusha waumini kuchanja, kutokana na ukweli kwamba, tangu ugonjwa uingie nchini, watu wamepotoshwa na kusababisha wasijue ukweli," alisema.

Mwenyekiti huyo alifafanua kuwa kutokana na mkanganyiko huo, wao huwa wanaelimisha waumini wao kuhusu umuhimu wa chanjo kuwa ni vyema kila mmoja aipate ili aweze kuwa salama.

"Kwa ujumla ni kwamba, upotoshaji huo kwamba chanjo ina madhara, umesababisha baadhi ya watu wasichanje baada ya kuambiwa kuwa wakichanjwa damu inaweza kuganda au kuwa wagumba," alisema.

Alisema, matarajio yao ni kuona waumini wengi zaidi wanapata chanjo, kwa kuwa uongozi wa parokia umeweka utaratibu wa kuwaita watoa chanjo ambao tayari walishafika kanisani hapo mara tatu.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (wapili kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Idara ya Huduma za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo, cheti cha shukrani kwa Benki ya NMB wakati wa hafla ya kuzipongeza timu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar baada ya kufanya vizuri katika mashindano ya mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Arusha. Kushoto ni Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuber Ali Maulid. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge lataka marekebisho sheria ndogo

**Na Salome Kitomari**

BUNGE limezitaka mamlaka zilizotunga sheria ndogo zinazokinzana na sheria mama kuzirekebisha haraka ili kuondoa usumbufu kwa wananchi, huku likitaka kuheshimiwa maelekezo ya muhimili huo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Jasson Rweikiza, akiwasilisha taarifa ya mwaka 2020/20, mwishoni mwa wiki, alisema walibaini baadhi ya sheria hizi zinakinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka kutungwa kwake au sheria nyingine za nchi, jambo linaloathiri tija ya utekelezaji wake na kuwa batili.

Alisema walibaini pia misingi ya uandishi bora wa sheria ndogo hauzingatiwi na kutaka mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga zirekebishe dosari hizo.

"Zipo sheria ndogo zilizowekwa mezani wakati wa Mkutano wa Tano wa Bunge ambazo hazikuzingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, jambo linaloondoa urahisi na kutabirika kwa sheria ndogo, hivyo kuathiri tija sheria," alisema.

Rweikiza alisema pia Bunge linaelekeza marekebisho ya haraka kwa sheria ndogo zilizotungwa ambazo masharti yake hayazingatii uhalisia na kuathiri utekelezaji na tija iliyokusudiwa.

Aidha, alisema Bunge limetaka mamlaka kukamilisha mchakato wa marekebisho ya sheria ndogo kwa ambazo zimechelewa kutekeleza maelekezo ya mhimili huo.

Alisema kuwa Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizobainika kutokuwa zimeanza utekelezaji wa mapendekezo ya muhimili huo yaliyohusu kurekebisha dosari katika sheria ndogo zitekeleze haraka na kutoa taarifa kabla ya kumalizika kwa Mkutano wa Saba.

Rweikiza alisema: "Bunge linaazimia kwamba, taasisi zinazotunga au kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria Ndogo, zishirikishe inavyostahili na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG)."

Alisema kamati ilibaini ushirikishwaji hafifu katika mchakato wa uwasilishaji licha ya kwamba AG ndiye mwenye dhamana ya uandishi wa sheria, hali iliyosababisha kuendelea kuwapo kwa dosari na usumbufu kwa watumiaji wake.

Alisema pia walibainia ushirikishwaji hafifu wa wadau kwa kuwa baadhi ya sheria hizo zimekosa mambo ya msingi kwa utekelezaji, na kuzuia upatikanaji wa mawazo jumuifu na kutatiza utekelezaji wake kutokana na manung'uniko ya wadau.

"Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo, zizingatie umuhimu wa kushirikisha wadau kikamilifu katika mchakato wa utungaji wa sheria hizo," alisema.

Wakichangia mjadala huo, Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo, alisema ni muhimu serikali inapoanza mchakato ishirikishe wadau ambao wako maeneo husika wanajua uhalisia.

"Umuhimu wa wadau ulionekana wakati tunataka kupitisha Sheria ya Tume ya Taaluma kwa Walimu na Sheria na Kanunuza Wavuvi, kote ilionekana wadau ni muhimu washirikishwe kwa kuwa kanuni iliyoruhusu samaki wenye urefu fulani wavuliwe Ziwa Victoria ilionekana kwa kina hicho hawapatikani Ziwa Tanganyika, baada ya kusikiliza wadau tuliona kuna umuhimu wa kuwasikiliza," alisema.

Mbunge wa Chakechake, Ramadhani Suleiman Ramadhani, alisema mwaka jana bunge liliopitisha azimio la kufanya marekebisho yenye dosari lakini hadi sasa hayajafanyika.

"Sasa ni mwaka serikali haijafanya marekebisho. Zipo sheria zinaumiza watu Bunge liliona likitaka marekebisho wamekuja na majibu yale yale huku wananchi wakiendelea kuumia. Mfano Halmashauri ya Mbeya Mjini kuna tozo za bajaji zilitakiwa kufanyiwa marekebisho ila hadi leo serikali iko kimya," alisema.

# Uzinduzi wa barabara ya Chuo cha Nyerere kesho

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAKATIBU wakuu kutoka vyama vya ukombozi Kusini mwa Afrika kesho wanatarajiwa kushiriki uzinduzi wa barabara ya lami yenye urefu wa kilomita mbili kwenda Chuo Kikuu cha Uongozi wa Siasa cha Mwalimu Julius Nyerere kilichoko Kibaha mkoani Pwani.

Barabara hiyo ambayo itazinduliwa na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, imejengwa na chama hicho kwa kushirikiana na Chama cha Kikomunist cha China (CPC).

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Kibaha, Katibu wa CCM Mkoa wa Pwani, Said Goha, alisema ufunguzi wa barabara hiyo ya Ukombozi ni maandalizi ya kukamilisha uzinduzi wa chuo hicho ambao utafanywa na Mwenyekiti wa CCM Taifa Rais Samia Suluhu Hassan.

Goha alisema katika uzinduzi wa barabara Chongolo ataambatana na makatibu wakuu hao kutoka vyama vilivyoshiriki ujenzi huo pamoja na wageni kutoka ndani na nje ya Mkoa wa Pwani.

Alisema chuo hicho ambacho kimejengwa na vyama vya Ukombozi Kusini mwa Afrika kitakuwa kinatoa maarifa kwa wanachama kujifunza mambo ya uongozi.

Aliwataka wanachama wa CCM kutoka katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo na wananchi kujitokeza kwa wingi kumpokea Rais Samia keshokutwa na kushiriki katika uzinduzi wa chuo hicho.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na kwamba ulinzi umeimarishwa kwa wageni watakaofika katika shughuli za uzinduzi wa barabara na chuo hicho.

Vyama vilivyoshiriki kujenga chuo hicho ni CCM (Tanzania), FRELIMO (Msumbiji), ANC (Afrika Kusini), SWAPO (Namibia), ZANU-PF (Zimbabwe) na MPLA (Angola).

# NMB yapewa kongole kufanikisha taasisi ya Mama Mariam Mwinyi

**Na Mwandoshi Wetu**, ZANZIBAR

BENKI ya NMB imetunukiwa cheti cha kuthaminiwa kwa mchango uliofanikisha uzinduzi wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), ambayo iliasisiwa na mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi.

Kutokana na hatua hiyo, benki hiyo imeahidi kukuza uchumi wa bluu unaochakatwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi.

NMB ilichangia fedha taslimu sambamba na 'track suit' na fulana 't-shirt' zilizovaliwa na washiriki wa matembezi ya kilomita sita kuanzia Viwanja vya Butroz Ghali hadi Mao Zedong, ulikofanyika uzinduzi wa taasisi hiyo inayojihusisha na Maendeleo Endelevu ya Wanawake, Vijana na Watoto, lengo likiwa kuunga mkono juhudi za SMZ katika kufanikisha ustawi wa makundi hayo kiuchumi, kiafya na kimaadili.

Cheti hicho kilitolewa na Mama Mwinyi na kupokelewa na Mkuu wa Idara ya Huduma za Serikali wa NMB, Vicky Bishubo, ambaye aliihakikishia ZMBF na Serikali ya Zanzibar, kuwa benki yake itaendelea kuwa mdau kiongozi na mtiifu katika kuunga mkono jitihada za kuleta maendeleo zenye nia ya kumkwamua Mzanzibari mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

"NMB hatuko nyuma. Chini ya Rais Hussein Mwinyi kwa mfano, tumeuunga mkono harakati za serikali yake kuchangia ukuaji wa uchumi wa bluu na leo tunamsapoti Mama Mwinyi na benki yetu itasimama naye hatua kwa hatua," alisema Bishubo akikumbushia udhamini wa NMB katika Zanzibar International Marathon na uzinduzi wa Kadi za Utalii Zanzibar (ZATO), zinazotumiwa na watalii visiwani humo.

Aidha, wakati Mama Mariam Mwinyi alipotembelea Banda la NMB kwenye uzinduzi huo katika Viwanja vya Mao, Bishubo alimsisitizia Mwenyekiti huyo wa Bodi ya Wadhamini ya ZMBF kuwa, kipaumbele chao ni uhusiano mwema baina ya taasisi zao, ambayo yatachagiza ufanisi katika kufikia malengo ya kusapoti jitihada za serikali inayohitaji nguvu za wadau katika kuharakisha maendeleo.

HABARI KITAIFA

# Bosi TANAPA aapishwa Dar

**Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro ameongoza kiapo cha utii cha Kamishna wa Uhifadhi - TANAPA, Mhifadhi William Mwakilema.

Hafla ya uapisho ilifanyika mwishoni mwa wiki katika jengo la Wizara ya Maliasili na Utalii maarufu kama Mpingo House, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya uapisho huo Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Francis Michael, aliahidi kuimarisha Jeshi la Uhifadhi na kuhakikisha kwamba linakuwa jeshi la kisasa.

Kwa upande, Mwakilema aliahidi pamoja na wahifadhi wenzake kuhakikisha wanalinda urithi wa maliasili zilizoko nchini sambamba na kufanyakazi kwa bidii na nidhamu.

"Kama ambavyo tumerithishwa maliasili hizi, naahidi mbele yako kwamba nitajitahidi kwa juhudi na maarifa kwa kushirikiana na wenzangu wote kuhakikisha kwamba ujuzi tulio nao, taaluma tulizo nazo, na kwakupewa fursa ya kutenda kazi kijeshi naamini kwamba wote tutakuwa na nidhamu ya hali ya juu ili kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu na kuweza kufikia malengo ya viongozi waliotutuma," alisema Mwakilema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya TANAPA, Jenerali mstaafu George Waitara, akizungumza katika hafla hiyo aliwakumbusha wahifadhi wote nchini kuendeleza nidhamu ya kijeshi inayotakiwa na kuhimiza ushirikiano kwa kiongozi huyo.

"Nahakika Kamishna Mwakilema akipata ushirikiano toka wizara, bodi na watumishi wenzake ataleta mafanikio ndani ya taasisi hii."

Kamishna Mwakilema amechukua nafasi ya Kamishna wa TANAPA, Dk. Allan Kijazi, ambaye sasa aliteuliwa hivi karibuni kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akimwapisha kiapo cha utii cha Kamishna wa Uhifadhi - TANAPA, Mhifadhi William Mwakilema, katika hafla ya uapisho iliyofanyika mwishoni mwa wiki katika ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii maarufu Mpingo House, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Skauti yapewa kongole uokoaji majanga ya moto

**Na Christina Mwakangale**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amekipongeza Chama cha Skauti Mkoa, kwa juhudi zake katika kushiriki shughuli za kijamii husussan kwenye majanga ya moto ikiwamo yaliyotokea soko la Mchikichini-Karume na Kariakoo.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, wakati akizungumza kwenye maadhimisho ya kumbukumbu ya Siku ya Mwanzilishi wa Skauti Duniani, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa, yaliyofanyika mkoani hapo.

Alisema mafunzo wanayopewa vijana wa skauti yanawajenga na kuwa na mbinu za kujitegemea na pia kuwaongezea ujasiri wa kuwafanya kushiriki shughuli kadhaa za kijamii ikiwamo uokoaji.

"Mimi mwenyewe (Gondwe) ni shahidi. Nimewakuta sana katika maeneo ya majanga mkitoa usaidizi. Mkuu wa Mkoa Makalla ameniagiza niwape pongezi kwa kujitoa kwenu kwenye mazingira yoyote, iwe jua au mvua," alisema na kuongeza:

Skauti yeyote katika jamii anakuwa ni wa kipekee iwe ni binti, kijana. Hii inajenga kuwa na vijana wa Kitanzania wazalendo, wenye nidhamu na wachapakazi."

Kadhalika, alitoa wito kwa wazazi na walezi kuwa tayari kuruhusu watoto wao kujifunza mafunzo hayo yanayowajengea uzalendo ambayo humwandaa mtoto kujua namna ya kujitegemea, kuwa na uamuzi kwa wakati sahihi tangu shuleni.

Akisoma risala ya Chama cha Skauti wa Dar es Salaam, Jensen Yona, alisema kwamba janga la UVIKO-19 lilisababisha changamoto kadhaa kwao, ikiwamo mwaka jana nchi kutoshiriki mkutano wa kimataifa, ambao hukutanisha nchi sita za barani Afrika, kila mwaka.

Yona alibainisha kwamba ushiriki wa skauti kwenye matukio ya kijamii husussan uokoaji, yameendelea kupewa kipaumbele na kwamba chama hicho kilishiriki kwenye majanga ya moto katika masoko yaliyoungua mkoani hapa hivi karibuni.

"Tunakabiliwa na ukosefu wa miradi, uhaba wa vifaa vya utendaji kazi kama vile mahema kwa ajili ya kutumika katika shughuli, tunaomba serikali itutambue kwa kuzingatia mchango wetu kwenye jamii," alisema Yona.

Naibu Kamishna Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania, Faustine Magige, alisema kumbukumbu ya kuzaliwa skauti hufanyika duniani kila Februari, na kwamba kaulimbiu ya mwaka huu nchini ni Shiriki katika Sensa ya Watu na Makazi Agosti 2022.

Kadhalika, alisema zipo baadhi ya athari zilizotokana na UVIKO-19 huku matukio kadhaa ya skauti yakilazimu kufanyika mtandaoni badala ya kukutana ana kwa ana kama ilivyo utaratibu wao kila wanapokutana huwezesha kufanya mazoezi kwa vitendo.

# Wenye ulemavu waiomba serikali kuwanunulia vifaa

**Na Lilian Lugakingira, MULEBA**

WENYE ulemavu mkoani Kagera wameiomba serikali kupitia halmashauri zote za wilaya, kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya kuwanunulia nyenzo za kujimudu kama fimbo nyeupe kwa wasioona, viti mwendo kwa wanaotambaa na shime sikio kwa viziwi.

Waliyasema hayo katika mafunzo ya kutambua haki zao za kupata matibabu bure, yanayofadhiliwa na Shirika la The Foundation for Civil Society,

Katibu wa shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu nchini (SHIVYAWATA) Mkoa wa Kagera, Sweetbert Mushangam, alisema kuwa wengi wao hawana uwezo wa kupata fedha kwa ajili ya kununulia vifaa hivyo, kutokana na hali ngumu ya kiuchumi inayowakabili.

"Wengi wetu kutokana na ulemavu tulionao tunashindwa kufanya kazi kikamilifu au kutofanya kazi yoyote, ni vigumu kupata fedha za kununua nyenzo za kujimudu, tunaomba angalau kila halmashauri iweke katika bajeti yake watu wenye ulemavu watano kila mwaka, wafadhiliwe vifaa hivyo," alisema Mushanga. Aidha, kuhusu suala la msamaha wa matibabu kwa kundi hilo aliiomba serikali kufikisha mwongozo wa utoaji wa huduma za afya kwa watu wenye ulemavu, katika vituo vyote vya kutolea huduma, ili waweze kutibiwa bure, kutokana na baadhi ya vituo kubainika kutokuwa na mwongozo huo.

"Lakini kila kata ihakikishe takwimu za watu wenye ulemavu na changamoto zinazomkabili kila mmoja wao zinapatikana kuanzia ngazi za vijiji, hii itasaidia kuwatambua na kurahisisha utoaji wa huduma kwao," alisema.

Naye Lawrian Protas, mmoja wa walionufaika na mafunzo hayo alisema katika masuala ya mikopo na miundombinu rafiki, wametajwa moja kwa moja, lakini kwenye afya wanatajwa wazee, wanawake wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, na watu wenye ulemavu hawatangazwi.

"Na sisi watu wenye ulemavu tunaomba tutangazwe moja kwa moja kwamba tuna msamaha wa matibabu, tuwekwe kwenye mabango kama ilivyo kwa makundi mengine, hii itatusaidia kupunguza vikwazo tunavyokumbana navyo tunapokwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya," alisema Protas.

Akijibu hoja hizo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Elias Kayandabila, alisema kuwa ni vigumu kuahidi kutoa huduma kwa kundi hilo kwa vitu ambavyo havikuwekwa katika bajeti, lakini akaahidi serikali kufanyia kazi baadhi ya changamoto zinazolikabili kundi hilo, kulingana na uwezo wa kifedha utaopatikana.

"Lakini sio kwamba serikali haifanyi kitu kwenu, tumekuwa tukifadhili mambo mbalimbali mfano kuwawezesha kushiriki makongamano yenu, ili mjadili kwa pamoja changamoto zinazowakabili, kwa lengo la kutafutiwa ufumbuzi," alisema.

Alisema bajeti za halmashauri hupangwa katika vikao vya maamuzi na kuwaasa kupitia vyama vyao kuwahamasisha watu wenye ulemavu kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi, ili wapate watu wa kuwawakilisha na kufikisha ipasavyo changamoto zinazowakabili.

"Ombi langu watu wenye ulemavu msiwe nyuma wakati wa chaguzi mbalimbali, maana ili mpate fursa ya kuingia katika vikao vya maamuzi, mfumo uliopo lazima muwe mmepita kwenye michakato ya kisiasa, mlizingatie hili kwa sasa litawasaidia kufanikisha sehemu ya mahitaji yenu," alisema.

Kuhusu matibabu bure kwa kundi hilo alisema kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Mwaka 2007 pamoja na mwongozo wa msamaha, vimetoa nafasi kwa sekta ya afya kutoa matibabu bure kwa makundi maalumu wakiwamo watu wenye ulemavu, na kwamba baadhi yao wamekwishanufaika na msamaha huo.

# SAGCOT yapokea ripoti za utafiti

**Mwandishi Wetu**

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) kimepokea ripoti za utafiti mbalimbali uliofanywa na vyuo vikuu sita duniani kikiwapo na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) zenye kuangazia umuhimu wa kuzingatia mipango mizuri ya matumizi ya ardhi na kilimo cha biashara.

Utafiti huo ulihusisha kongani za Kilombero na Ihemi. Akizungumza baada ya kupokea mawasilisho ya ripoti hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga, mbali ya kupongeza utafiti huo uliofanywa na vyuo hivyo, alisema lengo lao ni kuhakikisha wakulima wanazalisha kwa tija na uzalishaji sambamba na kuhimiza matumizi endelevu ya pembejeo bora ili kufikia malengo makubwa.

"Ninachukua nafasi hii kuvipongeza vyuo vyote vilivyofanikisha utafiti huo na ni wazi sasa kuwa malengo yaliyoainishwa kwenye tafiti hizi yanashabiiana na malengo yetu sisi kama SAGCOT jambo ambalo kwetu tunaliona kama litakuwa chachu kwa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini," Alisema Kirenga.

Aidha, aliwakumbusha wakulima kuwa na matumizi mazuri ya rasilimali ya ardhi ili kuleta malengo chanya kwenye sekta hiyo "Natoa rai kwa wakulima wadogo, wa kati na wakubwa kutumia vizuri rasilimali ya ardhi tuliyonayo ili ikatoe mchango chanya kwa Taifa."

Pia Kirenga alisema SAGCOT inafanya kazi kwa karibu na wadau kutoka serikalini, sekta binafsi na hasa mkulima mdogo ambaye ni mwekezaji mkubwa anayetegemewa siku zijazo.

"Utafiti huu ni mwendelezo wa matokeo ya ushirikiano wa SAGCOT na wadau mbalimbali katika kuinua sekta ya kilimo ili ikatoe mchango katika ujenzi wa Taifa," alisema Kirenga.

Naye Meneja wa SAGCOT kongani ya Kilombero, John Banga, alisema kikao hiko kimelenga kutoa elimu juu ya kuzingatia matumizi mazuri ya ardhi na kufanya kilimo biashara, lengo likiwa kuongeza tija katika uzalishaji.

"Matumizi bora ya ardhi na rasilimali zilizoko katika minyororo mbalimbali ya kilimo katika kongani ya Kilombero na Ihemi italeta chachu kwa wakulima kulima kilimo biashara kwa kulima eneo dogo na kuvuno mengi," alisema Banga.

Banga aliongeza kuwa wakati mwafaka kwa wadau na serikali kuzifikisha matokeo ya utafiti huo kwa walengwa ambao ni wananchi, ili ukatoe matokeo chanya ambayo yatamuinua mkulima.

Prof. Pantaleo Munishi kutoka SUA, alisema lengo la utafiti huo ni kuhakikisha wakulima wanalima kilimo chenye tija ambacho hakitoathiri mazingira na ikolojia.

"Utafiti huu umelenga kumsaidia mkulima kulima kilimo chenye tija ambacho hakitoathiri mazingira na ikolojia kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadaye," alisema Prof. Munishi.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara (DCB), Godfrey Ndalahwa (kushoto), akisalimiana na Ofisa Mkuu Mtendaji wa Kampuni ya Bima ya Alliance Life Insurance, Byford Mutimusakwa, katika uzinduzi wa DCB Skonga Klabu jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wapili kushoto ni Mkurugenzi wa Biashara wa DCB, Zacharia Kapama na Meneja wa Bima wa benki hiyo, Emanuel Kaganda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ahadi ya Mjema kumjengea mwanakijiji nyumba yatimizwa

**Na Marco Maduhu**, KISHAPU

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, ametimiza ahadi yake ya kumjengea nyumba ya kisasa, Mwashi Masanja (70), mkazi wa kijiji cha Ipeja wilayani Kishapu ambaye anasaidiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Januari 11, mwaka huu, Mjema alifanya ziara wilayani Kishapu ya kutembelea walengwa wa TASAF na kuona maendeleo yao ya maisha na alipofika kwenye kaya ya Masanja akamkuta anaishi kwenye nyumba ambayo siyo imara na kuahidi kumjengea nyumba nyingine.

Mjema alisema mlengwa huyo alikuwa anaishi na wajukuu zake wawili ambao bado ni wadogo kwenye nyumba ya tope licha ya kuezekwa kwa bati kupitia fedha za TASAF.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu huyo wa mkoa aliguswa na kuamua kutoa Sh. milioni 3.5, ili mwananchi huyo ajengewe nyumba nzuri ndogo ya kujistiri na wajukuu zake hao.

"Rais Samia Suluhu Hassan anataka tuwasaidie wananchi wake ambao wanaishi kwenye makazi duni hususani wazee na fedha hizi ambazo nimezitoa kujenga nyumba hii ya mlengwa huyu wa TASAF zinatoka kwake na leo namkabidhi rasmi nyumba yake ambayo nilimwahidi kumjengea," alisema Mjema.

"Nyumba hii ambayo nimemkabidhi mlengwa huyu wa TASAF ni ya chumba kimoja na ina umeme wa jua (Solar), tangi la kuhifadhia maji na ina choo cha kisasa," aliongeza.

Naye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) mkoani Shinyanga, Gaspel Kileo, alimuunga mkono Mjema na kumnunulia mlengwa huyo wa TASAF kitanda, godoro pamoja na mashuka ili awe analala mahali pazuri.

Diwani wa Kata ya Itilima wilayani Kishapu, Lameck Msubato, naye alimkabidhi mbuzi wawili mlengwa huyo wa TASAF, ambao atawafuga ili kumkwamua kiuchumi.

Kwa upande wake mlengwa huyo wa TASAF, alimshukuru Mkuu huyo wa Mkoa kwa kumjengea nyumba ya kisasa, ambayo ataishi yeye na wajukuu zake na kuwashukuru wadau wengine ambao wamemsaidia, huku akimwombea afya njema Rais Samia ili aendelee kuliongoza taifa vizuri.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, akisoma taarifa ya ujenzi wa nyumba hiyo ya mlengwa wa TASAF, alisema ulianza Februari 5, mwaka huu na kukamilika Feb 17 kwa gharama ya Sh. milioni 5.3 baada ya wadau wengine kutoa Sh. milioni 1.9 na yeye binafsi Sh. 400,000.

# Kafulila ahimiza utunzaji mitaro

**Na Happy Severine,** MASWA

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amewataka wakazi wa Mji wa Maswa mkoani humo kuitunza mitaro ya maji ya mvua inayojengwa kwenye baadhi ya barabara za mitaa ya mji huo.

Sambamba na kuitunza, amewasihi kuifanyia usafi wa mara kwa mara na kutotupa takataka ndani ya mitaro hiyo ili iweze kuwasaidia kusafirisha maji ambayo awali yalikuwa wakiingia kwenye nyumba zao hasa nyakati za mvua kunyesha.

Kafulila alisema haya jana, baada ya kutembelea ujenzi wa mitaro yenye urefu wa kilomita 5.5 inayojengwa kwenye mji huo chini ya wakala wa barabara mijini na vijijini (TARURA).

Aidha, amewataka makandarasi waliopewa kazi hiyo kukamilisha kwa wakati kama mikataba yao waliyosaini na TARURA Mkoa wa Simiyu inavyotaka kwani serikali imetoa fedha hizo kupitia tozo za mafuta na mfuko wa barabara.

Naye Meneja wa TARURA Wilaya ya Maswa, Mhandisi David Msechu, alisema kuwa wanatekeleza miradi mitano ya ujenzi wa mitaro hiyo yenye thamani ya Sh. 532,936,640.

Aliongeza kuwa miradi hiyo inatekelezwa kupitia kampuni mbalimbali ambazo ni MMETO CONSTRUCTION CO. LTD ya Dar es Salaam kwa gharama ya Sh. milioni 100.

Alitaja nyingine kuwa ni FRESAM CONSTRUCTION CO LTD ya Mwanza kwa gharama ya Sh. milioni111.2 na kampuni ya ASSA GENERAL SUPPLIERS AND CONSTRUCTION CO LTD ya Bunda, Mara kwa Sh. milioni 69.


Nyingine ni MORAJ WOMEN GROUP ya Shinyanga kwa gharama ya Sh. milioni 200 na Kampuni ya WAMAMA KAZI ya Tukuyu, Mbeya Sh. milioni 52.6.

Mhandisi Msechu alieleza kuwa unakabiliwa na changamoto ya kujengwa kwa miundombinu ya maji iliyokatisha au kupita sambamba na barabara ambayo imesimikwa kina kifupi kukatwa na kusababisha baadhi ya wananchi kukosa huduma ya maji ila wamekuwa wakishirikiana na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Maswa (MAUWASA) kuirejesha kwa wakati ili wananchi wapate huduma ya maji.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA PENALTI NYINGI KARNE YA 21 UK. 12


Neymar

# REKODI YA NEYMAR ILIYOWASHINDA MESSI, CR7

**LONDON, England**

HAKUNA shaka kwamba, Ronaldo Nazario de Lima ni mmoja wa wachezaji wakubwa zaidi ambao Brazil wamewahi kuwa nao. Alipata mafanikio mengi katika maisha yake ya soka, hata katika umri mdogo sana. Lakini Ronaldo alikuwa mzuri kiasi gani akiwa na umri wa miaka 21 na analinganaje na mastaa wanaochipukia wa siku hizi?

Kufunga mabao kwa mapenzi si jambo la maana na wachezaji kwenye orodha hii walikuwa na kipaji cha kufumania nyavu mara kwa mara. Hawa ndio wanasoka ambao walichukua ulimwengu kwa dhoruba tangu mapema sana katika maisha yao ya soka, kama Ronaldo alivyofanya.

Jambo la kushangaza ni kwamba Lionel Messi na Cristiano Ronaldo hawapo kwenye orodha hii, kwani walikuwa na mabao 51 na 36 kwa majina yao wakiwa na umri wa miaka 21. Wakubwa hao wawili bila shaka ni magwiji wa mchezo huo, lakini walichanua wakiwa wamechelewa kidogo katika maisha yao ya kifahari.

Kwa maelezo hayo, tuwatazame wanasoka watano waliofunga mabao mengi zaidi wakiwa na umri wa miaka 21, haya sasa...

**#5. Sergio Agüero: Mabao 84**

Sergio Aguero alianza safari yake ya soka akiwa na Atlético Independiente ya nchini Argentina. Baadaye alijiunga na Atletico Madrid mwaka 2006 na kuifanya dunia ikae kitako.

Aguero alishinda Ligi ya Europa akiwa na Atletico msimu wa 2009-10. Alijiunga na Manchester City mwaka 2011 na akaendelea kuunda historia kwenye Ligi Kuu ya England.

Aguero alikuwa na mabao 84 katika mechi 213 alipokuwa na umri wa miaka 21. Mabao mengi alifunga akiwa na Atletico Madrid. Kwa jumla, ana mabao 101 kwa timu hiyo ya Hispania. Aguero pia anachukuliwa kuwa mmoja wa wafungaji bora kwenye Ligi Kuu England. Muargentina huyo alifunga mabao 184 katika mechi 275 alizowachezea na anashika nafasi ya nne kwenye orodha ya wafungaji bora wa muda wote wa ligi hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alisajiliwa na Barcelona msimu uliopita wa joto, lakini kwa bahati mbaya aligundulika kuwa na ugonjwa wa moyo usio na ukomo muda mfupi baadaye. Aguero alitangaza kustaafu soka Desemba mwaka jana.

**#4. Erling Haaland: Mabao 113**

Erling Haaland tayari amejitambulisha kama mmoja wa washambuliaji mahiri kwenye mchezo huo. Idadi ya mabao ya raia huyo wa Norway ni ya kushangaza sana ikizingatiwa kwamba ana umri wa miaka 21 pekee. Uwezo wa Haaland ni wa kushangaza sana, na anaweza kuendelea kuwa bora zaidi ulimwenguni katika miaka ijayo.

Kinda huyo amefunga mabao 113 katika mechi 164 pekee. Alifunga zaidi ya nusu ya mabao hayo akiwa na Borussia Dortmund. Katika mechi 83 pekee katika mashindano yote, ana mabao 80 ya kushangaza kwa BVB.

Amefunga mara 16 katika mechi 14 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu huu, hata baada ya kukosa mechi chache kutokana na jeraha.

Ingawa Haaland hajajaribiwa kwenye ligi yenye ushindani zaidi, hakuna shaka juu ya uwezo wa kijana huyo. Klabu kubwa zote za Ulaya zinaitafuta saini ya kinda huyo mwenye umri wa miaka 21 katika dirisha lijalo la uhamisho wa majira ya joto.

**#3. Kylian Mbappe: Mabao 116**

Kylian Mbappe anaweza kuwa na umri wa miaka 23 pekee, lakini bila shaka ni mmoja wa washambuliaji wakubwa barani Ulaya. Mfaransa huyo tayari ameifungia klabu ya Paris Saint-Germain mabao mengi katika umri mdogo kama huu.

Mbappe alifikisha umri wa miaka 21 Desemba 2019. Mfaransa huyo alikuwa amefunga mabao 116 katika mechi 199 katika klabu na nchi akiwa na umri mdogo. Alikuwa mfungaji bora wa Ligue 1 kwa misimu mitatu kuanzia 2018-19.

Mbappé amefunga mabao 116 akiwa na umri wa miaka 21, mabao mawili tu pungufu ya Lionel Messi, Cristiano Ronaldo na Thierry Henry walikiwa wameunganishwa katika umri huo huo.

**#2. Neymar: Mabao 140**

Akiwa na ujuzi na udhibiti wa mpira wa kuvutia, Neymar ni mmoja wa wanasoka walio na kipaji cha kiufundi zaidi kwenye sayari hii. Neymar alipata umaarufu kule Santos na akachukuliwa haraka na Barcelona mwaka 2013.

Kufikia umri wa miaka 21, Neymar alikuwa amefunga mabao 140 katika michezo 227. Ronaldo Nazario de Lima pekee ndiye aliyefanikiwa kufunga mabao zaidi.

Neymar alikuwa katika kilele chake wakati alipokuwa Barcelona. Mbrazil huyo aliunda ushirikiano wa kutisha na Lionel Messi na Luis Suarez na kuifanya Barca kupata ushindi mara nyingi. Neymar alishinda mataji mawili ya LaLiga, moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya na matatu ya Hispania akiwa na Wakatalunya hao kabla ya kujiunga na PSG mwaka 2017 kwa ada ya uhamisho iliyovunja rekodi ya dunia ya Euro milioni 222.

**#1. Ronaldo Nazario: Mabao 167**

Washambuliaji wachache wameweza kuiga kipaji cha Ronaldo Nazario. Mbrazil huyo alifungua na kufafanua upya jukumu la mshambuliaji namba tisa.

Ronaldo ni miongoni mwa wachezaji wachache waliowahi kuwachezea wapinzani wao wawili katika ligi mbili tofauti. Alikaa mwaka mmoja Barcelona wakati wa msimu wa 1996-97 kabla ya kuhamia Inter Milan. Miaka mitano baadaye, alijiunga na Real Madrid kabla ya kujiunga na AC Milan mwaka 2007.

Rekodi ya ufungaji ya Ronaldo ya mabao 167 katika michezo 185 akiwa na umri wa miaka 21, ni ya aina yake. Mbrazil huyo alishinda tuzo yake ya kwanza ya Ballon d'Or mwaka 1997 alipokuwa na umri huo huo na ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kushinda tuzo hiyo ya kifahari.

Ronaldo aliendelea kushinda tuzo hiyo kwa mara ya pili mwaka wa 2002. Jambo la kushangaza ni kwamba Mbrazil huyo hajashinda kabisa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini ni mshindi mara mbili wa Kombe la Dunia.

## ISIKUPITE

CRISTIANO Ronaldo ndiye binadamu wa kwanza kutokea kuwa na wafuasi milioni 400 katika mtandao wa kijamii wa Instagram. Nyota huyo raia wa Ureno alifikisha idadi hiyo Februari 6, mwaka huu, ikiwa ni siku moja tu baada ya kusherehekea siku yake ya kuzaliwa akitimiza miaka 37.



## Extra Time

# WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA PENALTI NYINGI KARNE YA 21

**LONDON, Uingereza**

KARNE ya 21 imekuwa na mapinduzi katika soka kwa njia zaidi ya moja. Mtindo wa soka umebadilika msimu baada ya msimu na kasi yake inakuwa bora kadri muda unavyopita.

Jambo moja ambalo lilipaswa kuwa la kudumu limebadilika sana kwa njia yake yenyewe na ni sanaa ya kupiga adhabu. Wachezaji wamefafanua mitindo mipya na mbinu za kukaribia mkwaju wa penalti kwenye kisanduku.

Kinyume na imani ya kawaida, haijalishi ni rahisi vipi kufunga penalti. Shinikizo na ukali unaoizunguka hufanya iwe vigumu zaidi na wakati huo huo muhimu kuwa sahihi.

Wachezaji wengi katika karne ya 21 wamebobea katika sanaa ya kuwa wapigaji penalti waliofaulu. Kwa kuzingatia hilo, tuwatazame wanasoka walio na mabao mengi zaidi ya penalti kwa karne hii, twende sasa...

#10. Robert Lewandowski

Mshambuliaji huyo wa Poland amekuwa na mtindo wa ajabu mbele ya lango kwa takriban kila klabu ambayo ameichezea. Akianzia kucheza kule Lech Poznan, Robert Lewandowski alisajiliwa na Borussia Dortmund mwaka 2010.

Akiwa na mabao 103 katika mechi 187 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo ya Ujerumani, Mpolandi huyo ilikuwa vigumu sana kumzuia. Uchezaji wake uliendelea kuwa wa kiwango cha juu alipojiunga na Bayern Munich mwaka 2014.

Hadi sasa Lewandowski amefunga mabao 331 katika mechi 359 alizoichezea klabu hiyo ya Bavaria. Amefunga penalti 53 katika maisha yake ya soka hadi sasa na bila shaka atakuwa akiongeza zaidi kwenye hesabu zake kadri muda unavyokwenda.

**#9. Ronaldinho**

Wachezaji wachache sana katika historia ya soka wamefanya mchezo huo uonekane wa kufurahisha na rahisi kama Ronaldinho. Mshambuliaji huyo wa Brazil alifurahiwa kutazamwa akiwa dimbani.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2002 akiwa na Brazil, alichezea baadhi ya klabu za juu za Ulaya kama Paris Saint-Germain, Barcelona na AC Milan. Alipewa jukumu la kupiga penalti mara nyingi zaidi. Katika maisha yake ya soka, Ronaldinho alifunga mabao 57 kupitia mikwaju ya penalti.

**#8. Oscar Cardozo**

Sio wengi watafahamu aina ya mchezaji Oscar Cardozo. Mchezaji huyo wa Paraguay ni mshambuliaji mahiri mbele ya lango na umaliziaji wake mzuri.

Akiwa amecheza sehemu kubwa ya maisha yake ya klabu na Benfica, Cardozo alipata mafanikio mengi na klabu hiyo ya Ureno. Katika maisha yake ya soka hadi sasa, mshambuliaji huyo wa Paraguay amefunga mabao 58 na bado anaendelea vema akiwa na umri wa miaka 38.

**#7. Dusan Tadic**

Ilichukua muda kwa Dusan Tadic kupata kutambuliwa katika maisha yake ya soka. Akiwa amezichezea Vojvodina, Groningen na Twente kazi yake haikutambulika sana.

Alipofika Southampton katika Ligi Kuu England mwaka 2014, uchezaji wake ulivutia zaidi. Alijiunga na Ajax mwaka wa 2018 na tangu wakati huo amekuwa mchezaji mkubwa kwa upande wa Uholanzi, akifunga mabao 60 na kusajili asisti 61 kwenye Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, hadi sasa. Tadic amefunga mabao 58 ya penalti katika maisha yake ya soka kwa mguu wake wa kushoto.

**#6. David Villa**

Si wachezaji wengi wanaoweza kufunga bao la kujipinda kwa uzuri kama alivyofanya David Villa. Mhispania huyo alikuwa mshambuliaji wa kustaajabisha alipofanya maajabu kule Valencia kwa uwezo wake wa kumalizia.

Katika misimu yake mitano akiwa na klabu hiyo ya Hispania, alifunga mabao 107 katika mechi 167 za LaLiga. Baadaye alijiunga na Barcelona na kushinda ligi mara mbili akiwa nao. Katika maisha yake ya kuvutia ya soka, Villa alifunga mabao 60 ya penalti.

**#5. Ciro Immobile**

Mmoja wa wachezaji thabiti katika Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa miaka mingi amekuwa Ciro Immobile. Mshambuliaji huyo wa Kiitaliano amekuwa miongoni mwa wafungaji mabao mara kwa mara na bado alishindwa kutambuliwa kulikostahili.

Ukiondoa kipindi kirefu cha msimu akiwa na Borussia Dortmund na Sevilla, Immobile ametumia maisha yake ya klabu nchini Italia. Wakati wake bora umefika katika klabu yake ya sasa, Lazio. Akiwa ameshinda Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya katika msimu wa 2019-20, mshambuliaji huyo wa Italia amekuwa akistaajabisha mbele ya lango.

Katika mechi zake 248 akiwa na Lazio kwenye michuano yote, Immobile amefunga mabao 173 na kusajili asisti 45. Amefunga mabao 61 ya penalti katika maisha yake ya soka hadi sasa na kuna uwezekano wa kuongeza hesabu na kupanda daraja kwenye orodha hii kadri muda unavyokwenda.

**#4. Francesco Totti**

Miongoni mwa wachezaji wote kwenye orodha hii, Francesco Totti ndiye mchezaji pekee aliyecheza kwa muda muhimu katika karne ya 19. Hivyo inasemwa, alikuwa mchezaji wa klabu moja kwani aliichezea Roma pekee katika maisha yake yote ya klabu.

Kiungo huyo mkabaji alikuwa ni mtu wa kasi sana uwanjani na ubunifu. Gwiji huyo wa Roma alifunga mabao 307 katika mechi 785 alizoichezea timu hiyo ya Italia. Aliidhinishwa kupiga penalti mfululizo na alihusika katika kufunga mabao 73 ya penalti katika karne hii.

**#3. Zlatan Ibrahimovic**

Wachezaji huja na kuondoka lakini si wengi wanaoweza kufikia ujasiri na mafanikio ambayo Zlatan Ibrahimovic amekuwa nayo katika maisha yake ya soka. Mshambuliaji huyu wa Sweden amekuwa bora katika maisha yake ya soka ya kulipwa.

Amechezea klabu kubwa za Ulaya kama vile Ajax, Juventus, Inter Milan, Barcelona, AC Milan, Paris Saint-Germain na Manchester United. Mbinu bora ya Zlatan na uwezo wa ajabu wa kupachika mabao ni jukumu la yeye kufanikiwa karibu kila mahali alipokuwa akicheza.

Kwa klabu tisa alizochezea hadi sasa, nguli huyo amefunga mabao 467 na kusajili asisti 167 katika mechi 761. Ni mafanikio ya ajabu kutokana na ushindani kila mahali. Kufikia sasa, Ibrahimovic amefunga mabao 78 kwa njia ya penalti na anaweza kuongeza mengine kabla ya kutundika daluga lake.



Ronaldo

**#2. Lionel Messi**

Hakuna maneno mengi yanayoweza kutenda haki kwa ukuu wa Lionel Messi. Gwiji huyo wa Barcelona aliwashangaza wengi ilipothibitishwa kwamba atajiunga na Paris Saint-Germain katika dirisha la usajili la majira ya joto lililopita.

Akiwa amecheza misimu 17 na klabu hiyo ya Katalunya, kuondoka kwake bila shaka isingekuwa rahisi. Katika maisha yake ya hali ya juu akiwa na wababe hao wa Hispania, Messi alifunga mabao 672 katika mechi 778 kwenye mashindano yote.

Mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or anaweza kuwa anatatizika kidogo kwenye Ligue 1 hivi sasa, lakini anasalia kuwa mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote. Kufikia sasa, Messi amefunga mabao 78 kwa njia ya penalti, ambayo yote yamepatikana katika karne hii.

**#1. Cristiano Ronaldo**

Si rahisi kumruka Cristiano Ronaldo wakati mjadala wa mabao unafanyika. Nyota huyo wa Ureno amekuwa mtambo wa kupachika mabao katika maisha yake yote ya soka.

Bila kujali klabu, ligi au upinzani, Ronaldo ana uhakika wa mabao. Mshambuliaji huyo wa Ureno amekuwa mkubwa kwa umaliziaji wake wa kikatili na silika ya ajabu ya kufunga mabao. Katika maisha yake ya klabu, amefunga mabao 688 kwenye mechi 921 katika michuano yote.

Akiwa na mabao 128 ya penalti kwa jina lake katika karne ya 21, hakuna mchezaji aliyekaribia kumshinda Ronaldo katika suala hili. Inazungumza tu jinsi straika huyo wa Manchester United amejimudu katika hali kama hizi.

## Nukuu


"Lakini hatutakubali. Sitakuambia kuwa haiwezekani kuwakamata, lakini hakuna njia nyingine zaidi ya kuboresha mchezo na aina ya uchezaji wetu. Shinda mchezo baada ya mchezo, anza kushinda michezo mfululizo. Hakuna nafasi ya kuiangalia City au Liverpool au kuangalia nyuma," **Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel, akiamini kwamba anaweza kuishika Liverpool katika msimamo wa Ligi Kuu England baada ya kushinda bao 1-0 dhidi ya Crystal Palace juzi.**




"Changamoto ya kukaa muda mrefu bila kufunga humtokea mshambuliaji yeyote, kwa hiyo kwetu kama benchi la ufundi hatukuwa na hofu na uwezo wake [John Bocco] ndio maana tuliendelea kumwamini na kumpa nafasi ya kucheza na mwishowe sasa ameweza kufunga," **Kocha wa Simba, Pablo Franco baada ya Bocco kuanza kucheka na nyavu**



"Nimewahi. Sijui kama [itatokea kujiunga naye]. Lakini ndio, yeye ni kumbukumbu. Nilipokuwa mtoto nilikuwa nikitazama Barcelona ikishinda kila kitu na Ronaldinho, Xavi, Iniesta," **Kiungo wa Chelsea, Jorginho akielezea matamanio yake ya kucheza chini ya Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.**



# ‘SAVES’ TANO ZA HATARI RAUNDI YA 5 FA CUP




Kipa wa Yanga, Djigui Diarra, katika mazoezi ya kuokoa ‘michomo’.

**Na Adam Fungamwango**

RAUNDI ya tano ya Kombe la FA ilimalizika wiki iliyopita kwa timu nane kutinga hatua ya robo fainali.

Ni michuano ambayo bingwa huiwakilisha Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika. Awali hata aliyecheza fainali alikuwa na nafasi ya kuiwakilisha nchi kama bingwa wa FA atakuwa pia bingwa wa Ligi Kuu, lakini kwa sasa kanuni hiyo imebadilishwa na ikitokea hivyo, basi timu iliyoshika nafasi ya pili Ligi Kuu Bara ndiyo itakayoiwakilisha nchi.

Kwenye michuano hiyo imeshuhudiwa timu saba za Ligi Kuu zikitinga hatua hiyo, na moja ya Championship ambayo ni Pamba ya Mwanza, iliyoshangaza wengi kwa kuichapa Dodoma Jiji mabao 2-1.

Timu zingine zilizotinga hatua hiyo ni Geita Gold ilioichapa Mbuni bao 1-0, Azam FC ikiigaragaza Baga Friends mabao 6-0, Mabingwa Watetezi, Simba wakifanya mauaji ya mabao 7-0 dhidi ya Ruvu Shooting, wanafainali wa msimu uliopita, Yanga wakiiadhibu Biashara United mabao 2-0, Polisi Tanzania ikiichakaza Prisons mabao 2-0, Coastal Union ikitakata kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, na Kagera Sugar ikiidungua Namungo bao 1-0.

Kwenye hatua hiyo, baadhi ya magolikipa wameonekana kufanya vema na kuzibeba timu zao katika baadhi ya matukio kwa kuokoa hatari ambazo kwa asilimia kubwa zingeweza kuwa mabao.

Katika makala haya tumekusanya baadhi ya matukio ya hatari ambayo badhi ya makipa wamekumbana nayo na kufanya kazi ya ziada, tiririka nayo...

**Abdallah Jaffar - Baga Friends vs Azam**

Golikipa wa Baga Friends, Abdallah Jaffar, pamoja na kuruhusu wavu wake kutikiswa mara sita, wakipokea kipigo cha mabao 6-0 kutoka kwa Azam FC, Februari 12 kwenye mechi ya 32-bora ya Kombe la FA, aliokoa hatari moja ya maana ambayo kama asingefanya hivyo, basi timu yake yenye maskani yake mkoani Pwani ingepigwa mabao 7-0 kama Ruvu Shooting ilivyobugizwa na Simba, Februari 16.

Ilikuwa dakika ya 43, lilipotokea shambulizi kali, Paul Peter akipiga shuti kali lililowababatiza mabeki wa Baga Friends. Mpira huo ni kama ulimfuata Mudathir Yahaya ambaye alibaki hatua moja dhidi ya kipa huyo. Wakati wachezaji wa timu hiyo wakidhani ameotea, Mudathir alipiga mpira huo, lakini kwa ushahidi kipa huyo alichupa na kuucheza hapa na hapa, ikawa kona. Mechi hiyo ikichezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex. Chamazi, Dar es Salaam.

**Mohamed Hussein - Coastal Union vs Mtibwa**

Huyu ni kipa wa Coastal Union, ambapo kwenye mechi ya raundi ya tano ya Kombe la FA, aliokoa michomo miwili ya maana ambayo kama si hivyo huenda mechi hiyo ingeweza kuwa sare. Ilichezwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Februari 14, na Coastal ikashinda kwa mabao 2-0, na kutinga hatua ya robo fainali.

Mohamed Hussein aliokoa hatari ya kwanza ambayo ingeweza kuwapa bao Mtibwa Sugar sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko.

Steven Nsibamasabo aliwekewa pasi moja pembeni kidogo ya lango la Coastal. Akiwa hatua kadhaa na kipa, aliupiga mpira kwa kuukunja, akitaka kufunga kama alivyofanya Jimson Mwanuke kwenye mechi ya Simba dhidi ya Ruvu Shooting. Wakati Benedict Tinoko yeye alishindwa kwenda, Hussein alisafiri upande wa kushoto na kuupiga ngumi mpira ukawa kona na kuikoa timu yake.

Dakika ya 78 alifanya tena kazi ya ziada, baada ya kulazimika kutoka upande wa kushoto, na kuruka upande wa kulia, kupangua shuti kali lililopingwa pembeni na Salum Kihimbwa. Kihimbwa aliwapiga chenga mabeki kadhaa wa Coastal Union na nje kidogo ya eneo la hatari akiachia kombora kali eneo ambalo kipa hakuwa amesimama upande huo. Wakati wachezaji wa akiba na benchi la ufundi likisimama kujiandaa kushangilia, kipa huyo alizima ndoto hiyo.

**Ramadhani Chalamanda - Kagera Sugar vs Namungo**

Februari 14, ilichezwa mechi nyingine ya Kombe la FA, kati ya Kagera Sugar na Namungo kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera.

Kipa Ramadhani Chalamanda alifanya ‘save’ ya hatari dakika ya 56, kutoka kwa Abdulaziz Makame, ambaye alipata krosi safi kutoka kwa Reliants Lusajo.

Na kipa huyo alimsoma, Makame, kwani krosi hiyo ilitua kwenye kichwa cha Makame ambaye muda huo akiwa anapiga kichwa, Chalamanda alikwenda naye juu na kuweka mikono yake, hivyo mpira badala ya kutinga wavuni ukagonga kwenye mikono ya kipa huyo na kurejea uwanjani, Kagera Sugara ikishinda kwa bao 1-0.

**Djigui Diarra - Yanga vs Biashara**

Kipa raia wa Mali, Djigui Diarra naye hakuwa nyuma kwa makipa waliofanya kazi kubwa kwenye hatua ya raundi ya tano ya michuano ya Kombe la FA. Februari 15 Kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, moja ya ‘save’ ya maana aliyoifanya ni dakika ya 18, baada ya straika hatari wa Biashara United kuambaa na mpira kwenye winga ya kushoto, akaingia nayo ndani na kupiga krosi chonganishi ya chinichini na ya hatari.

Diarra alilazimika kutoka golini hatua moja na kuurukia mpira huo kama mkizi, kabla ya kuupangua kuurejesha uwanjani. Iwapo angesimama kusubiri ingewezekana kuwa bao, kwani wachezaji wawili wa Biashara United walikwenda moja kwa moja hadi wavuni baada ya kuukosa, ikionyesha kuwa walikuwa na kazi moja tu na mpira, huo, kuuweka kambani.

**JE, WAJUA?**



HARRY Kane wa Spurs na Carlos Tevez (enzi akiwa Man City) ndio wachezaji wa soka wanaoshikilia rekodi ya kutozwa faini kubwa kutokana na makosa mbalimbali (pauni 400,000) kuliko mchezaji yeyote yule, wakifuatiwa na Arda Turan ( pauni 350,000), Romelu Lukaku ( pauni 325,000) na Mario Balotelli (pauni 340,000).





Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi (katikati), akishuhudia Mkurugenzi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (kushoto), akimkabidhi Katibu Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi, Mathew Kirama, kompyuta kwa ajili ya wenye ulemavu wasioona, hawakutaja gharama na idadi za kompyuta walizokabidhi ofisi hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC Mtaka awapa wanafunzi jukumu kuikijanisha Dodoma

**Na Augusta Njoji,** MPWAPWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amezindua upandaji miti mkoani humo huku akiagiza kila mwanafunzi kuhakikisha anakuwa na mti wake shuleni ili kuikijanisha Dodoma.

Mtaka aliyasema hayo jana alipokuwa akizindua zoezi la upandaji miti na kuhamasisha kilimo cha mtama katika kijiji cha Kingiti wilayani Mpwapwa.

Alisema maofisa elimu wahakikishe miti inafika kila shule na kwamba kampeni inalenga kuhakikisha kila mwanafunzi anakuwa na mti.

"Hakikisheni mwanafunzi shuleni anasoma, ana eneo la kufanya usafi, mti anaoutunza, kuwa na bustani ya shule ili kupata elimu ya kupanda miti na utunzaji mazingira, nataka kuona vijiji Dodoma vyenye miti ya kivuli, miti chakula tupande miti yenye faida," alisema.

"Nataka tutengeneze kijiji tajiri cha mfano, shule tajiri, kijiji tajiri, watu tajiri kwa kupanda miti ya matunda na kivuli, pia WFP inahamasisha mlime mtama limeni kwa wingi," alisema.

Aliwataka Mameneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuhakikisha miti inapandwa kwenye barabara zinazojengwa na kuwataka wananchi kuondokana na tabia ya kupanda miti kiholela.

"Suala la kupanda miti kiholela tuachane nalo TARURA lazima mwonyeshe maeneo ya kupanda miti kila Barabara ya TARURA lazima kuonyesha eneo la kupanda miti," alisema.

Hata hivyo, alisema hayupo tayari kuona halmashauri inakimbizana kutoza wananchi ushuru wa mazao bila kuwekeza kwa kuwapa elimu na kuhamasisha kulima.

"Lazima kutoza kwa unachowekeza huyu anayetoza ushuru anajua maana ya kilimo na kuwa na mashamba, mtu anatoza Sh.1,000 hajui hata mkulima amehangaikaje, kuna siku nitawaambia msitoze, kama hamjawekeza kwenye kufanikisha kukusanya, ni lazima mkurugenzi kama una vijiji 10 vinakuletea Sh. bilioni tatu lazima uwekeze."

"WFP imetoa mafunzo kwa wakulima kulima mtama, sasa idara yako ya kilimo mkurugenzi imemfundisha nani, idara yako ya fedha imejiandaaje pale wananchi watakapozalisha mara 10 ya wanavyozalisha sasa au wakizalisha ndio mnaanza kusema hakuna pakuweka tukodi nyumba ya mtu," alisema.

Alitaka kuhakikisha suala la kuwekeza kwenye kilimo ili wanapokusanya ushuru uwe wenye tija kwao.

Kwa upande wa Mkuu wa Ofisi ndogo ya Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Nima Sitta, alisema pamoja na kuhamasisha upandani miti pia kuna vijiji 51 vinavyosaidiwa na WFP kupitia mradi wa mtama ambapo mwaka jana ziliuzwa tani 20,000 ambapo kati ya hizo tani 11,000 zilitoka Mpwapwa.

"Kwa Mkoa wa Dodoma kwenye mradi wa mtama tuna vijiji 222 kwenye wilaya zote na tunategemea mwaka huu tutafikia tani 50,000, kwenye miti tunajitahidi kurudisha ardhi tunayoitumia ambapo tumezalisha miti 62,000 ya asili, 6,000 ya matunda na Mpwapwa hapa wameshapanda miti 17,000," alisema.

# Huduma kibingwa zaipa nafuu hospitali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma imeondokana na upelekaji wagonjwa katika hospitali nyingine kutokana na maboresho yaliyofanywa na serikali kwenye huduma za kibingwa ambapo kwa sasa zipo zaidi ya 10.

Miongoni mwa huduma zinazotolewa katika hospitali hiyo ni pamoja na huduma za tiba kifua kikuu, masikio, pua na koo, macho, kinywa na meno pamoja na huduma za magonjwa ya wanawake na uzazi.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Ernest Ibenzi, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa juzi, alisema kuna madaktari bingwa 29 na wahudumu wengine wa afya ambao wanatoa huduma katika hospitali hiyo.

"Katika hospitali hii tuna mabingwa kutoka katika vitengo mbalimbali wapo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi na kuwafanya wanakuwa salama kiafya, tunashukuru serikali kwa kazi kubwa inayofanya haswa katika sekta ya afya nchini na kuiangalia kwa karibu Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma."

"Zamani tulikuwa tunawapeleka wagonjwa kupata huduma katika hospitali nyingine lakini kwa sasa huduma karibu zote na zile za kibingwa zinapatikana katika hospitali hii," alisema.

Alisema kuimarishwa kwa huduma katika hospitali hiyo imeleta mafanikio na mabadiliko makubwa kwenye sekta ya afya nchini na hivyo wananchi wa Dodoma na mikoa ya jirani hupatiwa huduma hizo Dodoma

Kwa upande wake, Dk. Samwel John, mtaalamu wa mifupa katika hospitali hiyo, alisema wanapokea wagonjwa waliopata ajali, waliotibiwa na kupata rufani kutoka ndani ya mkoa na mikoa jirani.

"Tunaishukuru serikali kwa kuboresha huduma pamoja na upatikanaji wa vifaa tiba/kinga kama vyuma na vifaa vya kutengenezea vifaa bandia," alisema.

# TASO yataka kurejeshwa viwanja vya maonyesho

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Wakulima nchini (TASO) kimeomba serikali kukirudishia viwanja vya maonyesho ya wakulima Nanenane ambavyo hivi sasa vinaendeshwa na mamlaka za mikoa kinyume na sheria.

Aidha, kimeiomba serikali kurudisha Maonesho ya Wakulima Nanenane ambayo yaliondolewa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo mwaka jana. Katibu Mkuu wa TASO Taifa, Herry Beji, alibainisha hayo jijini hapa akisoma tamko la Kamati Kuu Taifa kwa wajumbe wa mkutano mkuu maalum wa chama hicho.

Beji alisema pamoja na serikali kupoka mamlaka ya chama hicho kuviendesha viwanja vya maonesho ya wakulima maarufu kama Nanenane pia imechukua jukumu la kuratibu kazi zote zilizokuwa zikifanywa na TASO. Alisema, kutoka na hali hiyo TASO imeshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na rasilimali zote ambazo chama kilikuwa kikitegemea kujiendesha kupokwa na mamlaka za mikoa.

"Tunaiomba serikali kuturudishia viwanja vyetu ambavyo tulikuwa tunaviendesha sisi kama Chama cha Wakulima, lakini iturudishie jukumu letu la kuendesha maonyesho ya wakulima Nanenane ambayo sisi ndiyo tunahaki nayo kwa mujibu wa taratibu," alisema Beji.

Alivitaja viwanja hivyo kuwa ni kiwanja cha maonesho ya wakulima nanenane Nzuguni cha jijini Dodoma, Nanenane Morogoro, Mbeya, Arusha pamoja na Lindi.

"Viwanja hivi vyote vitano vilikuwa vinaendesha na TASO, na shughuli zote za maonesho sisi ndiyo tulikuwa tunaratibu kwa kuwa ndiyo wenye shughuli hii ya wakulima lakini kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo serikali imepoka mamlaka haya," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini TASO Taifa, Said Amanzi, alisema mwaka 2017, chama hicho kilipokonywa usajili kutokana na changamoto zilizokuwapo wakati huo.

"Wakati ule ambapo TASO, ilifutwa serikali ilichukua jukumu la kuratibu shughuli za TASO, kwa muda na jukumu lilikabidhiwa kwa mamlaka za mikoa, lakini sasa chama tayari kimerudishiwa usajili na wenzetu wa mikoa hawataki kurudisha viwanja na wengine wameanza kubadili hata umiliki wa viwanja," alisema Amanzi.

Kadhalika, alisema kutokana na hali hiyo ya kupokwa viwanjwa na mamlaka ya kuendesha shughuli zote za nanenane wamekosa nguvu za kukiendesha chama na kusaidia wakulima kufikia malengo yao.

"Ili Tanzania kufikia azma yake ya uchumi wa viwanda ni lazima TASO itekeleze majukumu yake kwa kusaidia wakulima katika maonyesho, elimu pamoja na mafunzo ili hivyo viwanda vipate malighafi kutoka katika mazao ya kilimo na mifugo," alisisitiza Amanzi. Mdhamini wa TASO, Nyanda za Juu Kaskazini, Kapteni Mstaafu Nkoswe Noel, alisema serikali inatakiwa kukaa meza moja na chama hicho cha wakulima kwa ajili ya mslahi mapana ya wakulima na taifa kwa ujumla. "Serikali itusaidie ili tuendelee kuwasaidia wakulima Watanzania kupata fursa ya mafunzo ya kilimo na fursa za maonyesho ya Nanenane na iturudishie mamlaka yetu kama ambavyo wafanyakazi wanavyokuwa na siku yao ya Mei mosi na sisi turatibu wenyewe siku ya wakulima nanenane na wao tuwaalike tuu kuja kutoa maelekezo yao,"alisema Noel.



# BoT yafafanua muda wa sarafu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imesema kila sarafu inayochapishwa na benki hiyo ina muda wake wa kuwapo kwenye mzunguko.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa Idara ya Sarafu wa BoT, Ilulu Said Ilulu, wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari za biashara na uchumi yaliyoendeshwa na benki hiyo jijini Mbeya.

Hata hivyo, Ilulu alisema sarafu nyingi huwa hazifiki muda huo na badala yake huchakaa mapema na kuondolewa.

Alisema noti ya Sh. 10,000 ndiyo inakaa kwenye mzunguko kwa muda mrefu kuliko noti zote kwa maelezo kuwa inatakiwa kukaa mwaka mmoja na miezi tisa, 5,000 inatakiwa kukaa mwaka mmoja na miezi saba, 2,000 miezi 11 na 1000 miezi 10.

Alisema Sh. 500, 200, 100 na 50 zinatakiwa kuwapo kwenye mzunguko kwa muda wa miaka 26, lakini nazo hazifiki kwa sababu ya utunzaji mbovu unaofanywa kwenye mzunguko.

Alisema asilimia kubwa ya sarafu hizo hazifiki muda huo unaotarajiwa kutokana na utunzaji mbovu wa wananchi ikiwamo kuzikunja, kuzichana na wakati mwingine kuzilowanisha.

"Sera ya BoT ni kuhakikisha sarafu zinazokuwa kwenye mzunguko ni zile safi pekee, chafu zote zinaondolewa na kuharibiwa kwenye matawi yetu, tujitahidi kuwaelimisha wananchi wawe wanatunza vizuri sarafu hizi," alisema Ilulu.

BoT iliandaa mafunzo ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari za biashara, uchumi na fedha 43 wa vyombo mbalimbali kutoka mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi na Zanzibar.

Katika hatua nyingine, BoT ilivishauri vyombo vya habari kusaidia kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko nchini ili kuvutia wawekezaji kwa lengo la kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Kaimu Ofisa Uhusiano na Itifaki wa BoT, Vicky Msina, alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya alipokuwa anafunga mafunzo hayo ya siku tano na kufafanua kuwa vyombo vya habari ni mdau muhimu kwenye masuala ya uchumi, hivyo ni muhimu kushirikiana na wadau kwenye kutangaza fursa mbalimbali zinazopatikana za uwekezaji.

Alitaja baadhi ya sekta zenye fursa kubwa ya uwekezaji kuwa ni kilimo hasa cha maparachichi, madini, uvuvi na utalii na kwamba waandishi wa habari wanatakiwa kuandika habari zinazohamasisha uwekezaji kwenye sekta hizo.

Alisema benki hiyo itakuwa tayari kushirikiana na waandishi wa habari hasa kuwasaidia maofisa wake ambao ni wataalamu wa masuala ya uchumi na fedha kufafanua baadhi ya mambo ambayo waandishi watakuwa wanahitaji ili wananchi waelewe vizuri.

Vilevile aliwaomba waandishi wa habari kusaidia kuwaelimisha wananchi kuhusu utunzaji sahihi wa sarafu ili kupunguzia serikali hasara ya uchapishaji wa sarafu hizo mara kwa mara baada ya kuziondoa kwenye mzunguko zinazoharibika.

# RC kuwashtaki TANROADS kwa waziri

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amekerwa na utendaji kazi mbovu wa Wakala wa Barabara (TANROADS) hasa kwenye matengenezo ya barabara, hivyo wajitathmini kama wanatosha kwenye nafasi zao.

Aidha, ametishia kuwachukulia hatua za kiutendaji maofisa wa wakala huo endapo watashindwa kutekeleza maelekezo ya serikali, huku akitishia kumwandikia barua Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, kuhusu utendaji wa maofisa hao.

Homera alieleza alikerwa na utendaji wa wakala huo mwishoni mwa wiki alipoambatana na kamati ya ulinzi ya mkoa huo kwenye ziara ya kukagua barabara ya Mbeya - Tabora, ambayo maeneo mengi hayapitiki kipindi cha mvua.

Homera alisema maofisa wa TANROADS walimwahidi Oktoba mwaka jana kwamba wangeanza kuifanyia matengenezo barabara hiyo siku 10 baada ya siku aliyokutana nao, lakini haijafanyiwa chochote.

Alisema wananchi wamekuwa wakipata shida ya usafiri kutokana na baadhi ya maeneo magari kushindwa kupita hali inayosababishwa na ubovu wa barabara hiyo, lakini maofisa hao wameshindwa kuifanyia marekebisho.

Alisema awali aliwahoji maofisa hao kwanini hawakuifanyia matengenezo kiangazi, lakini wakamjibu kuwa inatakiwa kujengwa masika kutokana na kiangazi maji kutopatikana kabisa katika maeneo mengi ya barabara hiyo.

"Wenzetu kule Singida wanafanya vizuri sana, barabara wanaijenga kwa kiwango kizuri, lakini ninyi huku mnakwangua kwangua, na nina taarifa hapa mmepewa zaidi ya Sh. bilioni 1.4 za matengenezo lakini hakuna kinachofanyika, sasa mjitathmini," alisema Homera.

Aliwataka maofisa hao kuacha urafiki na mkandarasi aliyepewa zabuni ya kuifanyia matengenezo barabara hiyo kwa maelezo kuwa urafiki huo ndio unaosababisha washindwe kumsimamia vizuri.

Alisema hivi karibuni wakati wa maadhimisho ya miaka 45 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Mara, alimwomba Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba apite barabara hiyo na kwamba alimweleza kuwa hali ni mbaya.

Awali Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, alisema barabara hiyo ni mbovu katika maeneo mengi na inahatarisha maisha ya wananchi wanaoitumia pamoja na usalama wa vyombo vyao vya moto.

Alisema kwa sasa kusafiri kutoka Chunya mjini kwenda Makongolosi ni rahisi kwa sababu tayari barabara hiyo imejengwa kwa kiwango cha lami, lakini kuanzia hapo kuelekea Lupa barabara ni mbovu na haifanyiwi matengenezo ya kuridhisha.

"Tunakuomba Mkuu wa Mkoa utusaidie maana wananchi wetu wanateseka, huu ukanda una uchumi mkubwa sana kwa taifa, ni ukanda ambao kilimo cha tumbaku kinafanyika kwa kiwango kikubwa," alisema Mwanginde.

Katika hatua nyingine, Homera alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, kutumia vyombo vyake vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi wa ujenzi wa barabara hiyo ili hatua zichukuliwe.




Mafuriko yakiwa yamevamia makazi ya watu katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya baada ya mifereji ya barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kushindwa kuhimili maji ya mvua mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Busokelo, Rungwe kutathmini ruhusa za watumishi wanaokwenda kusoma

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

MAOFISA Utumishi wa Halmashauri za Rungwe na Busokelo wameagizwa kufanya tathmini kuhusu ruhusa za watumishi wanaoomba ruhusa za kwenda masomoni kutokana na baadhi yao kuzitumia vibaya nafasi hizo.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alitoa agizo hilo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Busokelo ambapo alisema baadhi ya watumishi wamekuwa wakiitumia vibaya nafasi hiyo na kusababisha upungufu wa watumishi.

Aliwataka maofisa hao kufuatilia ili kuhakiki kama kweli kila mtumishi anayeomba ruhusa huwa anaenda kusoma kama ambavyo huwa wanaomba na kwamba kwa wale watakaobainika wanadanganya wanatakiwa kuchukuliwa hatua.

Alisema kuna baadhi ya idara zimekuwa zikikumbwa na upungufu wa watumishi kutokana na wengi wa wanaokuwa wamepangiwa kufanya kazi kwenye idara hizo kuomba ruhusa ya masomo.

"Fanyeni tathmini ili tujuwe kama kweli hawa watu wanakwenda kusoma, idara nyingi ukifuatilia zinaonekana zina upungufu wa watumishi kutokana na wengi wao kwenda kusoma," alisema Dk. Anney.

Katika hatua nyingine Dk. Anney aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kushirikiana na watendaji wa halmashauri kubuni vyanzo vya mapato na kuvisimamia ili kuongeza mapato.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busokelo, Anyosisye Njobelo, alisema ili kuhakikisha wanaongeza ukusanyaji wa mapato wametunga baadhi ya sheria ndogo ambazo wanasubiri kibali cha waziri ili waanze kuzitekeleza.

Alizitaja sheria hizo kuwa ni sheria ndogo ya ada ushuru pamoja na ushuru wa huduma, na kwamba madiwani wamezipitisha kwa pamoja na wanasubiri zipitishwe na waziri.





# Ushirikiano TCCA na wadau usafiri wa anga kukuza uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Baraza la Ushauri wa Utumiaji Huduma za Anga Tanzania (TCCA), Shaabani Mtambalike, amesema ushirikiano kati ya baraza na wadau wa masuala ya anga utawezesha kuimarisha huduma za usafiri wa anga na kukuza uchumi.

Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa wadau wa masuala ya anga Mjini Zanzibar.

Alisema hatua hiyo pia itawezesha wadau hao kuwa huru katika kutoa mawazo ya huduma zinazotolewa ili kukidhi mahitaji ya wageni wanaoingia nchini.

Aidha, alisema miongoni mwa mambo muhimu katika kukuza soko la usafiri wa anga ni mfumo mzima wa kutatua malalamiko ya watumiaji ikiwamo utunzaji mizigo hivyo wadau wataweza kutoa mawazo namna bora ya huduma zinaendelea kutolewa katika viwanja vya ndege hasa vya Tanzania na Zanzibar.

Naye Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Innocent Kyara, alisema sekta ya utalii Zanzibar ni sehemu kuu ya uchumi ambapo hutegemea matumizi ya anga, hivyo ipo haja kuona inatafutwa njia bora ya kuimarisha huduma nzuri ili kuongeza idadi ya wageni na kukuza uchumi wa Zanzibar.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kukusanya maoni ambayo yatasaidia katika kuboresha sekta hiyo na kuishauri serikali maeneo ambayo yanasaidia katika kuboresha sekta hiyo.

Kwa upande wao washiriki wa mkutano huo walisema bado ipo haja ya taasisi hiyo kutoa elimu kwa wananchi juu ya kutambua haki na matumizi ya viwanja vya ndege na kutambua sehemu husika ya kufikisha malalamiko yao ili yaweze kupatiwa ufumbuzi.

Rashid Abdalla Salum, msimamizi wa kazi kitengo cha maelekezo na utangazaji Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar na Selwa Ali Sheha kutoka TCCA, walisema mafunzo hayo ni muhimu kwani abiria wanapopata changamoto hawajui suluhisho lao.

Walisema hatua hiyo itawasaidia wao na wananchi wa Zanzibar na hata wageni wanaoingia nchini kuhusu matatizo yanayojitokeza mara kwa mara ya usafiri wa anga na kuona yanatatuliwa haraka.



Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said (katikati), akizungumza na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Makazi, Joseph Kilangi (kulia) na Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Shabani Khamis, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wanawake wamkosha Spika kwenye uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatambua na kuheshimu mchango wa wanawake katika uongozi ili kuleta tija katika nchi.

Naibu Spika wa Baraza hilo, Mgeni Hassan Juma, aliyasema hayo wakati akisoma hotuba kwa niaba yake alipokuwa akizindua mafunzo ya mwanamke kiongozi kwa wajumbe wanawake wa Baraza la Wawakilishi.

Alisema mchango wa wanawake katika uongozi ni mkubwa na utafiti mbalimbali umeonyesha kuwa unaleta tija katika maendeleo.

Aidha, alisema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ameonyesha nia thabiti kwa kuteua wanawake mahiri kushika nafasi mbalimbali zenye umuhimu mkubwa katika nchi.

Aidha, alikipongeza Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Waajiri la Norway (NHO) pamoja na Chuo cha Uongozi cha ESAMI kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sio tu katika masuala ya usawa wa kijinsia mahala pakazi, bali pia kwenye masuala yanayohusiana na kazi na ajira.

Naye Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, alisema uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, na ushiriki wao kwenye siasa, ni kigezo muhimu katika kuhakikisha usawa wa kijinsia.

Aliahidi kuwa Norway itaendelea kuipa kipaumbele ajenda ya usawa wa kijinsia, na kuwatetea wanawake katika masuala ya uongozi na wapo tayari kushirikiana pamoja na Zanzibar ili tuimarishe mustakabali wa wanawake.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Suzanne Ndomba Doran, alisema tangu kuanzishwa kwa programu hiyo mwaka 2016, jumla ya wanawake 201 kutoka katika taasisi na kampuni 59 wamepatiwa mafunzo hayo na kuhitimu.

Aidha, alisema wengi waliopita katika mafunzo hayo wamefanikiwa kushika nafasi za juu za uongozi katika taasisi mbalimbali pamoja na bodi za wakurugenzi.

# SMZ: Tunatambua umuhimu wataalamu TEHAMA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesema inatambua umuhimu wa kuwa na wataalamu wa teknolojia ya TEHAMA wabobezi kwa maslahi ya maendeleo ya Taifa.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, alieleza hayo katika hafla ya ufunguzi wa semina ya wataalamu wa TEHAMA Mjini Zanzibar.

Waziri Rahma alisema serikali zote mbili zimewekeza kwa kiasi kikubwa katika kutoa elimu ya TEHAMA kulikowezesha kuzalisha wataalamu ambao kutokana na mabadiliko ya kasi wanahitaji kuendelezwa ili kukabiliana na vikwazo katika maendeleo ya TEHAMA.

Alieleza kuwa mbali na kuendeleza wataalamu wa TEHAMA, SMZ kupitia wizara hiyo, imekuwa ikitoa ushirikiano wa kutosha katika kukuza ubunifu na utafiti mbalimbali katika TEHAMA.

Aidha, alipongeza juhudi za Tume ya TEHAMA kwa kuanza kusajili wataalamu wa tasnia hiyo wakiwamo kutoka Zanzibar ambao wameanza kunufaika na mpango (programu) za tume za kuwaendeleza kupitia mafunzo na kubadilishana ujuzi na uzoefu.

"Ninahimiza waajiri wote ikiwamo serikali kama mwajiri mkuu kuanza kutumia wataalamu wa TEHAMA waliosajiliwa," alisema Waziri Rahma.

Alifafanua kuwa kufanya hivyo katika kuweka mkazo kupitia TEHAMA itaiwezesha nchi kuendana na mabadiliko katika uchumi wa dunia ambao matumizi ya TEHAMA ni makubwa yamepiga hatua.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Amour Hamil Bakar, alieleza kuwa katika zama hizi TEHAMA ni nyenzo muhimu kwa kuiwezesha jamii kushiriki ipasavyo katika uchumi wa kidijital (Digital Economy).

Pia alisema TEHAMA imetoa fursa mbalimbali ikiwamo kufanya biashara za kibenki kwa njia ya simu na internet pamoja na kufanya shughuli za kila siku (e.bussiness).

"Nawaombeni wataalamu wa TEHAMA tuitendee haki taaluma yetu ili kuirahisishia serikali shughuli zake za kiutendaji," alisema Bakar.

Alisema katika kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanaongezeka kwa jamii ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, serikali imejenga vituo 10 kwa lengo la kutoa elimu na kuwasogezea karibu huduma hizo wananchi walioko katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Simson John Mwel, alieleza kuwa pamoja na maendeleo yaliofikiwa lakini kuna athari kubwa inaweza kujitokeza kwa taifa endapo nchi haitakuwa makini kwa kuwatambua wataalamu wake ikiwamo kutokuwa na uhakika wa usalama wa mifumo ya TEHAMA pamoja na kutegemea wataalamu kutoka nje ya hali ambayo italigharimu Taifa fedha nyingi.

## Wakulima kahawa kugawiwa miche 3,000,000 bure

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya JJAD Kagera Farmers (T) kwa kushirikiana na Bodi ya Kahawa nchini (TCB), inatarajia kugawa miche 3,000,000 ya kahawa aina ya robusta bure kwa wakulima kama motisha.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya JJAD, Dk. Albert Katagira, alisema hayo, mwishoni mwa wiki kuwa wanatarajia kugawa miche hiyo kwa wakulima kuanzia wiki hii kama hatua ya kuwapa motisha wakulima waendelee kulima zao hilo kwa wingi.

Alisema tukio la kugawa miche hiyo kwa wakulima litafanyika katika Kijiji cha Karenge Tarafa ya Kaisho Wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera na aliomba wakulima hao wajitokeze kwa wingi kuchangamkia fursa hiyo.

Wakati huo huo, taarifa iliyotolewa na TCB iliwataka wakulima kuchangamkia fursa hiyo ili wapate miche bora ya kahawa itakayowasaidia kwenye kilimo bora.

Ilisema miche hiyo bora iko tayari kwa ajili ya kwenda shambani mwezi huu hivyo hiyo itakuwa fursa kwa kila mkulima wa zao hilo.

Oktoba mwaka jana Kampuni ya JJAD Kagera Farmers (T), ilishinda tuzo ya kuwa uzalishaji bora wa kahawa nchini kwa mwaka 2021.

Mashindano hayo yaliyoendeshwa na TCB, yalifanyika mwaka jana wilayani Moshi Mkoa wa Kilimanjaro.

Kwenye mashindano hayo yaliyoshirikisha sampuli 68 za kahawa kutoka mikoa mbalimbali nchini, JJAD iliibuka kidedea kwenye kahawa aina ya Robusta kwenye nafasi ya pili na ya tatu baada ya tathmini kufanyika.

Mashindano hayo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuwahamasisha wakulima kulima kahawa iliyo bora zaidi.

Dk. Katagira alisema kwenye mashindano yaliyomalizika hivi karibuni zili𝑙etwa sampuli 68 na kisha kufanyiwa tathmini ya ubora na wataalamu wa TCB na ndipo JJAD iliibuka mshindi kwa upande wa kahawa ya robusta.

Alisema JJAD ni kampuni inayozalisha na kuuza kahawa nje ya nchi ambapo inamashamba ekari zaidi ya 100 wilayani Kyerwa mkoani Kagera.

Dk. Katagira alisema katika kuboresha ubora wa kahawa, JJAD imeingia mkataba na TCB kwa ajili ya kuzalisha miche bora ya kahawa ya robusta ambayo inatija kwa asilimia 100 kulinganisha na miche ya zamani.

Alisema mche mmoja wa mbegu bora ya Robusta unauwezo wa kuzalisha kilo 2.5 ya kahawa kwa mwaka wakati ile ya zamani uwezo wake ni kuzalisha nusu kilo kwa mwaka.

Alisema mipango yao kwa mwaka uliopita wa 2021 ulikuwa kuzalisha miche milioni 1.5, mwaka 2021-2022 miche milioni 3 mwaka 2022- 2023 miche milioni 4.5, mwaka 2023-2024 miche milioni sita na mwaka 2024-2025 miche milioni saba.

# Bunge labaini shida shamba sukari NSSF

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

BUNGE limesema limebaini usimamizi mbaya wa shamba la mradi wa kuzalisha sukari la Mbigiri, Dakawa mkoani Morogoro, huku thamani ya mali za Jeshi la Magereza iliyokadiriwa ikiwa chini kuliko uhalisia.

Mradi huo uko chini ya kampuni hodhi ya Mkulazi iliyoundwa kwa ushirikiano baina ya Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) Septemba 6, 2016.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki bungeni jijini Dodoma alipowasilisha taarifa ya mwaka 2020/21.

Alisema taarifa ya ukaguzi wa ufanisi wa mradi wa kuzalisha sukari katika shamba la Mbigiri imebainisha dosari kadhaa ikiwamo usimamizi mbaya wa shamba na kutosimikwa kwa kiwanda.

"Dosari hizo zimesababisha hasara kwa wabia wa mradi (NSSF na Jeshi la Magereza) na wakulima wadogo wa miwa wa maeneo ya Dakawa," alisema.

Kaboyoka alisema Bunge linaitaka serikali kutekeleza kikamilifu mapendekezo 12 yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika taarifa ya ukaguzi wa ufanisi ili malengo ya mradi yafikiwe.

Mbunge huyo wa Viti Maalumu alisema lengo kuu la kampuni ni kuzalisha sukari nchini, NSSF ikiwa na hisa asilimia 96 na Magereza asilimia nne.

"Pamoja na kuzalisha sukari yenye ubora, kampuni ilitarajiwa pia kuzalisha bidhaa zinazotokana na miwa.

"Ili kufikia lengo hili kampuni ilipanga kutekeleza miradi miwili ya sukari ambayo ililenga kuzalisha tani 250,000 za sukari kwa mwaka," alisema.

Aliongeza kuwa shamba la Mkulazi wilayani Morogoro Vijijini, lilianzishwa kwa lengo la kuzalisha tani 200,000.

"Ripoti ya CAG imebainisha masuala kadhaa katika utekelezaji wa mradi wa uzalishaji sukari katika eneo la Mbigiri, yanatakiwa kufanyiwa kazi kwa haraka ili kuhakikisha malengo ya mradi yanafikiwa.

"Kuna upungufu katika usimamizi wa shughuli za shamba. Mathalani, kulikuwa na visima vyenye thamani ya Sh. milioni 81.5 vilichimbwa, lakini vilichelewa kuanza kutumika," alifafanua.

Kaboyoka alisema kulikuwa na matumizi ya mbolea na viuatilifu bila kuwa na maelezo ya matumizi yake, ucheleweshaji wa ujenzi wa kiwanda cha sukari na usimikaji wa mitambo pamoja na dosari kwenye usimamizi wa shughuli za ununuzi na mikataba.

Kaboyoka alisema Kampuni ya Mkulazi haijasajiliwa ili kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa mujibu wa sheria.

**MGAWANYO WA HISA**

"Hoja nyingine ambayo ukaguzi wa ufanisi umeibua ni kuhusu mgawanyo wa hisa uliowasilishwa katika taarifa za fedha za Kampuni ya Mkulazi.

"Mapitio ya nyaraka za makubaliano ya ubia ya Oktoba 17, 2020 kati ya Bodi ya Wadhamini ya NSSF na Magereza ambao watachangia kwa thamani ya mali za Sh. bilioni 19.380.

"Uchambuzi zaidi katika taarifa ya ukaguzi wa ufanisi ulibainisha kuwa thamani ya mali hizo ambazo zilichangiwa na Jeshi la Magereza zilikuwa ni zaidi ya asilimia nne ya kiasi cha mtaji wa ubia kilichoidhinishwa cha Sh. bilioni 250," alisema.

Kaboyoka alisema ukokotozi halisi wa kiwango cha mtaji uliochangiwa ni asilimia 7.6 ya mtaji wa ubia ulioidhinishwa.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kamati ilibaini hoja ya mgawanyo sahihi wa hisa kwa kuzingatia kiasi halisi cha mali kilichochangiwa na wanahisa, inahitaji kufanyiwa kazi na wanahisa kabla ya mradi kufikia hatua kubwa ya utekelezaji.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania PLC, Sitholizwe Mdlalose (watatu kulia), Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia (wapili kulia) na maofisa wengine wa kampuni hiyo baada ya Vodacom kukabidhi kompyuta na tablets kwa shule za Mkoa wa Kilimanjaro ikiwa ni sehemu ya uzinduzi wa mradi wa uunganishwaji wa shule kidigitali, katika hafla iliyofanyika Shule ya Sekondari Mawenzi Manispaa ya Moshi, hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake waonyeshwa fursa za madini

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

SERIKALI imewataka wanawake kuchangamkia fursa katika sekta ya madini kwa kipindi hiki ili kuongeza mitaji waliyonayo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alipotembelea mgodi wa kati wa Canuck Mining Company Limited ulioko Kijiji cha Numbi, Kata ya Mwakata Halmashauri ya Msalala kukagua shughuli za maendeleo.

Alisema kuwa katika Wilaya ya Kahama leseni 600 zimetolewa na Wizara ya Madini kwa ajili ya uchimbaji, huku akiwataka wanawake kuwa mstari wa mbele katika kuwekeza sekta hiyo.

Alisema kuwa katika Wilaya ya Kahama kuna baadhi ya wanawake wameingia katika sekta ya madini na kuanza kumiliki shughuli mbalimbali zikiwamo za uchimbaji.

"Kwa sasa sisi kama serikali ya wilaya tunawakaribisha wawekezaji hususani wanawake kuwekeza katika sekta ya madini kwani maeneo ya uwekezaji yapo na leseni zipo za kuwawezesha kufanya shughuli hizo za uchimbaji katika wilaya yangu," alisema.

Kiswaga alisema kuwa ardhi iliyoko katika maeneo ya Kahama ni ya mheshimiwa Rais na muda wowote kwa mtu ambaye atakuwa tayari kuwekeza katika madini anaweza kufika katika mamlaka husika kwa ajili ya kufuata taratibu za uwekezaji katika eneo ambalo atakuwa ameridhika nalo.

Meneja Rasilimali Watu wa mgodi huo, David Deogratius, alisema katika mgodi wake wa dhahabu wameajiri wanawake kwa asilimia 30.

Aidha, Deogratius alisema kuwa mgodi huo umekuwa chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi wanaozunguka katika eneo hilo na kwamba wanatoa ajira kwa wanakijiji wanaozunguka eneo hilo la uchimbaji.

Alisema awali walipata shida kuhamisha wachimbaji wadogo waliokuwapo katika eneo hilo na kufikia uamuzi wa kuwalipa Sh. milioni 10 kwa kila mmoja kama kifuta jasho.

Aliongeza kuwa hadi kufikia Februari, mwaka huu, jumla ya wafanyakazi 227 wameajiriwa na vibarua 40 na kwamba wanaume wapo 245 na wanawake 22.

Kampuni ya Canuck inaundwa kwa ubia wa kampuni mbili za Kiranova Investment Company Limited iliyosajiliwa nchini Sylichels na Lilac Baobab Capital Limited iliyosajiliwa nchini Tanzania kwa ajili ya kuendesha uchimbaji wa dhahabu katika eneo hilo.

# Ethiopia yaanza kuzalisha umeme megawati 5,000 kutoka Mto Nile

**Addis Ababa, ETHIOPIA**

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, amezindua rasmi chanzo cha uzalishaji umeme kupitia Mto Nile, kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha zaidi ya megawati 5,000 kikiwa kikubwa barani Afrika.

Abiy, aliambatana na maofisa kadhaa walipotembelea kituo cha uzalishaji umeme jana, na kubonyeza kitufe cha ishara ya uzinduzi huo.

Kituo hicho chenye mitambo 13 kiitwacho Grand Ethiopian Renaissance Dam (GERD), kilianza uzalishaji umeme jana, kwa kuanzia kuzalisha megawati 375 katika mtambo mmoja.

"Kuanzia sasa kutakuwa hakuna ambacho kitazuia Ethiopia kuzalisha umeme huu. Chanzo hiki kimejemgwa na Ethiopia ila si kwa ajili yetu tu, ni kwa ajili ya kaka, dada zetu Waafrika, watanufaika na mradi huu," alisema Abiy.

Mradi wa GERD, ambao ni mkubwa ukitumia bwawa la maji barani Afrika, ingawa nchi jirani za Ethiopia ikiwamo Sudan na Misri, zikisema kwao mradi huo kwao ni kikwazo kwa sababu wanategemea Mto Nile kwa shughuli mbalimbali.

Pia mradi huo unakadiriwa kugharimu Dola bilioni 4.2 unatarajia kuzalisha megawati 5,000 ikiwa ni mara mbili ya ule nchi ya Ethiopia inaouzalisha sasa.

"Tumeanza uzalishaji lakini haimaanishi kwamba mradi umekamilika," alisema Kifle Horo, Meneja Mradi GERD, aliongeza: Itatuchukua miaka miwili au mitatu kukamilisha kabisa.

***Alarabiya News/AP***



Waokoaji wakiwa eneo la Jiji la Petrópolis nchini Brazili, kutafuta manusura na miili ya waliofunikwa na kifusi, ikiwa ni siku ya nne tangu mafuriko yalivyosababisha maporomoko ya udongo na kuua takribani watu 200. **PICHA: BBC**

# Johnson: Ushahidi upo Urusi kupanga vita

**Munich, UJERUMANI**

"USHAHIDI unaonyesha kuwa Urusi inapanga vita kubwa zaidi barani Ulaya tangu 1945," Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amesema.

Johnson alimwambia mwandishi wa BBC Sophie Raworth katika mahojiano: "Ishara zote ni kwamba mpango huo tayari kwa maana fulani umeanza."

"Ujasusi unapendekeza kwamba Urusi inakusudia kufanya uvamizi ambao utauzingira mji mkuu wa Ukraine Kyiv," Johnson alisema.

"Watu wanapaswa kuelewa gharama kubwa katika maisha ya binadamu ambayo inaweza kutokea," aliongeza.

Waziri mkuu huyo, alikuwa akizungumza kutoka Munich, ambapo viongozi wa dunia wanakutana katika mkutano wa kila mwaka wa usalama.

Makadirio ya hivi punde ya serikali ya Marekani yanaonyesha, kati ya wanajeshi 169,000 na 190,000 wa Urusi, wako kwenye mpaka wa Ukraine nchini Urusi na nchi jirani ya Belarus, ingawa idadi hiyo pia inajumuisha waasi Mashariki mwa Ukraine.

Johnson pia alionyesha kwamba Uingereza italeta vikwazo vikubwa zaidi dhidi ya Urusi kuliko ilivyopendekezwa hapo awali.

Alisema Uingereza na Marekani, zitazuia makampuni ya Kirusi kufanya biashara ya pauni na dola, hatua ambayo aliitaja itaipiga sana nchi hiyo.

Vikwazo vya awali vilivyopendekezwa na mawaziri ni pamoja na kupanua wigo wa watu wa Urusi na biashara ambazo Uingereza inaweza kulenga.

Maofisa wa nchi za Magharibi, wameonya katika wiki za hivi karibuni kwamba Urusi inaweza kujiandaa kuivamia wakati wowote, huku Urusi ikikanusha madai hayo, ikisema wanajeshi wanafanya mazoezi ya kijeshi katika eneo hilo.

Alipoulizwa ikiwa uvamizi wa Urusi bado unafikiriwa kuwa karibu, Johnson alisema: Ninaogopa kwamba ndivyo ushahidi unavyoelekeza. Ukweli ni kwamba dalili zote ni mpango upo tayari kwa maana fulani umeanza."

Waziri Mkuu alisema Rais wa Marekani, Joe Biden, aliwaambia viongozi wa nchi za kijasusi wa nchi za Magharibi kwamba, vikosi vya Urusi havikuwa vinapanga tu kuingia Ukraine kutoka Mashariki, kupitia Donbas, ila kutoka Belarus na eneo linaloizunguka Kyiv.

"Ninaogopa kusema kwamba mpango tunaouona ni wa kitu ambacho kinaweza kuwa vita vikubwa kabisa barani Ulaya tangu 1945 kwa kiwango kikubwa," waziri mkuu alisema.

"Watu walihitaji sio tu kuzingatia uwezekano wa kupoteza maisha ya Waukrani, lakini ya Warusi vijana," aliongeza.

Johnson alikuwa akizungumza baada ya kukutana na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky na kuwaambia viongozi wa dunia katika hotuba yake kwamba uvamizi wowote wa Ukraine unaofanywa na Urusi "utalaaniwa kote duniani".

***BBC***

# Mahakama ICJ kusikiliza kesi mauaji Warohingya

**Naypyitaw, MYANMAR**

MAHAKAMA ya Kimataifa ya Haki (ICJ), leo, itaanza tena kusikiliza kesi ya mauaji ya kimbari dhidi ya jamii ya walio wachache ya Rohingya nchini Myanmar.

Kesi hiyo inaanza kusikilizwa katikati ya hoja kuhusiana na iwapo watawala wa kijeshi nchini Myanmar watalazimika kuhudhuria wakiliwakilisha taifa hilo la Asia ya Myanmar.

Kesi hiyo itakayosikilizwa kwa siku nne kuhusiana na mapingamizi ya awali ya Myanmar kwenye kesi hiyo iliyowasilishwa na Gambia kwa niaba ya jumuiya ya mataifa ya Kiislamu yanayoituhumu Myanmar kwa mauaji hayo ya kimbari na hatua kali dhidi ya jamii ya Rohingya.

Agosti mwaka 2017 jeshi la Myanmar lilianzisha kile kilichoitwa kampeni ya safishasafisha katika jimbo la Rakhine kujibu shambulizi la kundi la waasi wa jimbo la Rakhine.

Watu zaidi ya 700,000 walilazimika kukimbilia nchi jirani ya Bangladesh na kuanzisha madai dhidi ya vikosi vya usalama ya ubakaji, mauaji na kuchoma moto makazi yao.

**DW**

# Uingereza yarejesha Nigeria mali zake zilizoibwa tangu ukoloni

**Lagos, NIGERIA**

UINGEREZA imerejesha vitu vya thamani vilivyoibwa na wanajeshi wake nchini Nigeria, hatua inayoibua matumaini kwamba maelfu ya kazi za sanaa zilizoibwa huenda sasa zikarejeshwa katika makazi yake ya asili.

Shaba hizo zilirudishwa kwenye kasri la kitamaduni nchini humo.

Vifaa hivyo vya kiasili vilivyopelekwa zaidi barani Ulaya, viliibwa na wakoloni kutoka kwa iliyokuwa Ufalme wa Benin ambayo sasa ni Kusini Magharibi mwa Nigeria na ni miongoni mwa urithi muhimu wa kitamaduni barani humo ambao kulingana na makumbusho ya Uingereza zilitengenezwa karne ya 16.

Hii ni hatua kubwa katika harakati za Afrika za kurejesha nyumbani mali zilizoibwa katika enzi ya ukoloni, wakati wanahistoria wa kazi za sanaa wa Ufaransa wakisema karibu asilimia 90 ya kazi hizo ziko Ulaya.

**DW**

# JOHNNIE WALKER KUENDELEA KUSAIDIA MAENDELEO GOFU

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti Limited (SBL), kupitia kinywaji chake cha Johnnie Walker, imesema itaendelea kusaidia maendeleo ya mchezo wa gofu hapa nchini.

SBL kupitia kinywaji cha Johnnie Walker, imekuwa mstari wa mbele katika kusaidia maendeleo ya mchezo wa gofu ikiwa ni pamoja mashindano makubwa kuliko yote hapa nchini ya Waitara Trophy yanayofanyika kila mwaka katika viwanja vya Gofu Lugalo jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, amenukuliwa wakati wa hafla ya kutoa zawadi kwa washindi wa mashindano ya Johnnie Walker Waitara Trophy 2022, akisema kuwa kampuni yake ni mdau mkubwa wa michezo ikiwa ni pamoja na mchezo wa gofu.

"Hii ni mara ya pili kwa kinywaji chetu maarufu duniani cha Johnnie Walker kudhamini mashindano haya makubwa. Mwaka jana tulikuwa ndiyo wadhamini wakuu kama ilivyo kwa mwaka huu pia," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kinywaji cha Johnnie Walker ambacho kinasherehekea miaka 200 tangu kuanza kuuzwa, kinayo furaha kuwa sehemu ya mashindano hayo makubwa hapa nchini ambayo yaliwaleta pamoja zaidi ya wachezaji 200 wa gofu kutoka ndani na nje ya nchi.

Gofu ni moja kati ya michezo yenye historia kongwe duniani. Mchezo huu ulianza takriban miaka 600 iliyopita na kwa sasa unakuwa kwa kasi huku ukichezwa na watu wa kariba tofauti.

Aidha, mchezo huu pia umekuwa ukitoa mchango mkubwa wa kiuchumi kupitia ajira kwa vijana wanaofanya kazi katika viwanja vyake pamoja na kukuza na kutangaza utalii kupitia wageni wanaokuja na kuucheza nchini.

Meneja Masoko wa SBL, Lumuli Minga, aliongeza kuwa, kinywaji hicho kinadhamini mashindano katika klabu maarufu za gofu hapa nchini ikiwa ni pamoja na Dar es Salaam na Arusha Gymkhana Club, Lugalo Gofu Club pamoja na Sea Cliff Golf Club ya Zanzibar.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Bregedia Jenerali mstaafu, Michael Luwongo, ambao ndiyo waandaaji wa mashindano ya Johnnie Walker Waitara Trophy, ameishukuru Kampuni ya SBL kupitia kinywaji cha Johnnie Walker kwa kudhamini mashindano hayo kwa mara ya pili mfululizo.

"Gofu ni mchezo ambao ulikuwa haupewi kipaumbele sana kwenye suala la udhamini kama ilivyo mchezo wa mpira wa miguu na kwa maana hiyo umekuwa haukuwi kwa haraka. Kuja kwa Johnnie Walker kumeweza kuunyanyua na sasa unaenda vizuri," alisema.

Kampuni ya Bia ya Serengeti ni mdau wa michezo mingine ikiwamo mpira wa miguu. SBL ndiyo mdhamini wa timu ya Taifa, Taifa Stars na pia ndiyo mdhamini wa kwanza na wa pekee kwa Ligi Kuu ya Wanawake nchini.



Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Bregedia Jenerali mstaafu, Michael Luwongo, akimkabidhi zawadi ya kikombe Meneja Masoko wa SBL, Lumuli Minga, ikiwa ni ishara ya shukrani kwa udhamini wa mashindano ya Waitara Trophy 2022. **MPIGAPICHA WETU**

## Ngairo awika timu ya wenye ulemavu Uturuki

**Na Saada Akida**

NYOTA Mtanzania, Frank Ngailo, anaendelea kufanya vizuri katika majaribio yake ya kucheza soka la kulipwa nchini Uturuki katika Klabu ya Izmir BBSK kwa kufunga mabao matatu katika michezo mitatu na kutoa mchango wa mabao saba kati ya tisa waliyofunga hadi sasa.

Ngairo yupo Uturuki kwa majaribio huku akiendelea kupewa nafasi ya kucheza mechi katika klabu hiyo inayoshika nafasi ya tano kwenye Ligi Kuu ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ngairo alisema mchezo ambao timu yake ilishinda mabao 3-0 dhidi ya Kornya alifunga bao moja na kuhusika katika hayo mengine mawili na kuifanya klabu hiyo kuendelea kupata matokeo mazuri katika ligi hiyo.

Alisema mchezo wa pili walishinda 5-0 dhidi ya Malaysia, huku akicheka na nyavu mara mbili na kuhusika kutoa pasi ya mwisho moja na mechi ya tatu walishinda 1-0 akiendelea kuhusika na bao hilo lililowapa pointi tatu katika mchezo huo.

"Nafurahi kuendelea kufanya vizuri na kocha wa hii timu ameniamini na kunipa nafasi kwa sababu michezo yote nilicheza dakika 90," alisema Ngailo.

Alisema anapata nafasi ya kucheza katika kikosi cha kwanza kwa sababu kocha amemwamini pia ni miongoni mwa watu ambao wamempendekeza kwenda Uturuki kufanya majaribio katika timu hiyo.

"Nina matarajio makubwa na maendeleo ninayoendelea kuyaonyesha kwa kumshawishi kocha kunipa nafasi ya kusajiliwa ndani ya timu hii na kucheza soka la kulipwa," alisema Ngailo.

Mbali na Ngailo pia kiungo Mtanzania anayecheza timu ya Taifa ya Tanzania "Tembo Warriors", Ramadhani Chomelo yuko mbioni kujiunga na Klabu ya Konya EGSK inayoshiriki Ligi Kuu ya Wenye Ulemavu nchini Uturuki.

Chomelo atakuwa mchezaji wa pili kutoka Tanzania kucheza soka la kulipwa barani Ulaya baada ya Ngairo na kwa sasa klabu hiyo inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu Uturuki.

## Minziro ataja siri ya ushindi Geita Gold

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Geita Gold, Filex Minziro, amesema usajili alioufanya ndani ya kikosi chake kimeleta chachu ya ushindani, jambo ambalo linakifanya kikosi chake hicho kifanye vizuri kwenye Ligi Kuu ya NBC msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Minziro alisema mikakati yake ni kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa ligi hiyo inayojumuisha timu 16 msimu huu.

"Mikakati yangu ni kushika nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC," alisema Minziro ambaye ndiye aliyehusika kuipandisha Ligi Kuu msimu huu.

Aidha, alisema anafurahishwa na nidhamu inayoonyeshwa na wachezaji wake ndani na nje ya uwanja, pamoja na kufuata kwa umakini maelekezo anayowapa huku akieleza pia 'kukunwa' na pointi tatu walizozipata kwa kuilaza Coastal Union mabao 2-0 juzi.

Alisema licha ya mchezo huo kuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa wachezaji wake walijitahidi kupata matokeo hayo chanya.

## Vita vya maafande Ligi Kuu Zanzibar leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MIAMBA miwili ya soka visiwani Zanzibar, timu ya Maafande wa Zimamoto na Maafande wa JKU, itakutana leo kwenye Uwanja wa Amaan majira ya saa kumi alasiri katika mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar wakati huu ikiwa mzunguko wa 19.

JKU wanashuka dimbani wakiwa na alama 36 zinazoifanya kushika nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo wakati Maafande wa Zimamoto wakiwa nafasi ya sita baada ya kujikusanyia pointi 30 hadi sasa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohmed Hilali 'Tedy', alisema amekiandaa kikosi chake kuhakikisha kinapata alama tatu ili kusonga mbele na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa kuwa JKU inaendelea kuzichanga vema karata zake ili kujiimarisha katika nafasi za juu na kuukaribia ubingwa na wao, Zimamoto wanataka kuhakikisha wanakuwa katika nafasi tatu za juu.

"Lengo letu ni kuwa mabingwa wa Ligi Kuu, lakini kwanza lazima tuhakikishe tunakuwa katika nafasi tatu za juu tukitokea nafasi ya sita, ili tufanikiwe hilo lazima kuhakikisha (mchezo) huu tunapata alama tatu," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY, STERLING KUTETA
MANCHESTER City inapanga mazungumzo ya mkataba mpya na Raheem Sterling mwishoni mwa msimu huu, lakini wanaweza kuamua kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kama hawatafikia muafaka. ***(Times via City Xtra)***

### CHELSEA WAMSUBIRI CESAR
CHELSEA imemwambia Cesar Azpilicueta watamsubiri mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, kuamua majaliwa yake. Mlinzi huyo wa kimataifa wa Hispania amepewa ofa ya mkataba wa miaka miwili na Barcelona huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja. ***(Fabrizio Romano)***

### DALOT KUBAKI UNITED
MLINZI wa Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 22, anataka kuongeza mkataba wa kumbakiza Manchester United, na kufanya majaliwa ya mlinzi wa kulia, Aaron Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 24 kuwa shakani. ***(Star)***

### MORATA AWANIWA ARSENAL
ARSENAL wanataka kumsajili straika wa Hispania, Alvaro Morata mwenye umri wa miaka 29, huku Atletico Madrid wakiwa tayari kumuuza. Kwa sasa Morata anacheza kwa mkopo kule Juventus. ***(Tuttomercato)***

### DALOT ATAKIWA FIORENTINA
KLABU ya Fiorentina imeripotiwa kuwania saini ya Diago Dalot, lakini wanatakiwa kumshawishi mlinzi huyo wa pembeni kupunguza mshahara wake ili wamsajili. ***(La Nazione via Sportwitness)***

### RONALDO HATAZUIWA KUSEPA
MANCHESTER United hawatamzuia mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 kama atataka kuondoka mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### BIESLA KUONDOKA LEEDS
KOCHA wa Leeds United, Marcelo Bielsa mwenye umri wa miaka 66, anapanga kuondoka klabuni hapo kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### GBAMIN ATAKIWA SCKA
KIUNGO wa Everton na Ivory Coast, Jean-Philippe Gbamin mwenye umri wa miaka 26, anawaniwa na CSKA Moscow na anaweza kuondoka kwanza kwa mkopo. ***(Liverpool Echo)***

### BABA KUMHAMISHA HAALAND
BABA wa straika wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland, ambaye ni mchezaji wa zamani wa Leeds na Manchester City, Alf-Inge Haaland, anafanya kazi kubwa kuhakikisha uhamisho wa mwanawe huyo mwenye umri wa miaka 21, unakamilika kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### CHELSEA YAMWINDA MILITAO
CHELSEA wanapanga kumsajili mlinzi wa Real Madrid na Brazil, Eder Militao mwenye umri wa miaka 24. ***(Marca)***

### CARVALHO KUTUA UNITED
MANCHESTER United wanaweza kuwazidi akili Liverpool na kumsajili mchezaji, Fabio Carvalho mwenye umri wa miaka 19, kutoka Fulham kipindi cha majira ya joto wakati mkataba wake utakapofikia mwisho. ***(Star)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MAN CITY, LIVERPOOL SASA MBIO ZA FARASI WAWILI EPL

●●●Kipigo cha City kwa Spurs chatoa nafasi kwa miamba ya Anfield wenye mchezo mmoja mkononi kuwania taji hilo, huku...

**LONDON, England**

JUMAMOSI ilikuwa siku ya aina yake kwenye Ligi Kuu England (EPL), na matokeo ya mshtuko yakiathiri ncha zote za msimamo kuanzia juu, katikati na mkiani.

Liverpool wanaonekana kuwa wapinzani tena wa moja kwa moja katika mbio za ubingwa baada ya ushindi wao wa mabao 3-1 dhidi ya Norwich City na kufuatiwa na ushindi wa Tottenham Hotspur wa 3-2 ugenini dhidi ya viongozi Manchester City.

Mohamed Salah alifunga bao lake la 150 kwa Liverpool naye Luis Diaz akafunga bao lake la kwanza katika soka la Uingereza, huku mchezaji anayelengwa na City, Harry Kane akiwaadhibu 'Wananchi' hao pale kwenye Uwanja wa Etihad.

Kwingineko, bao la dakika za majeruhi la Hakim Ziyech liliihakikishia Chelsea ushindi dhidi ya Crystal Palace, wachezaji vijana wa Arsenal wakipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Brentford, huku West Ham wakilazimishwa sare ya 1-1 na Newcastle katika mchezo wa mapema.

Burnley waliwashangaza wengi kwa kushinda 3-0 dhidi ya Brighton, huku Watford pia wakitoa kipigo cha 1-0 kwa Aston Villa katika mechi ya aina yake.

Mchezo mwingine wa ligi hiyo ulishuhudia Southampton wakiilaza Everton ya Frank Lampard 2-0 pale St Mary's shukrani kwa mabao ya Stuart Armstrong na Shane Long.

Kikosi cha kocha Pep Guardiola cha City kilionekana kuwa kwenye kiwango kibovu zaidi kwa mara ya kwanza tangu kilipopoteza nyumbani dhidi ya Crystal Palace Oktoba mwaka jana.

City walikuwa watawala kwenye mchezo huo, lakini umakini wao mdogo ukawafanya Spurs kutumia nafasi chache walizopata kujihakikishia ushindi.

Spurs walipata ushindi huo kwa mashuti manne pekee kati ya 21 yaliyolenga lango.

Bao la ushindi la Kane, lililowekwa kimiani dakika ya 94:25 na likawahakikishia ushindi. Lilikuwa bao la 'jioni' zaidi la ushindi kufungwa dhidi ya City kwenye Ligi Kuu England tangu Michael Owen alipofanya hivyo na Manchester United Septemba 2009, akifunga dakika ya 95:27.

Wachezaji wawili wa Tottenham, Kane na Son Heung-min sasa wamesaidiana kwa mabao 36 ya Ligi Kuu, idadi kubwa zaidi ya upatina kwa wawili katika historia ya ligi hiyo, wakizidi upatina wa Didier Drogba na Frank Lampard.

Son amehusika moja kwa moja katika mabao 10 katika mechi 15 dhidi ya City (mabao saba, asisti tatu); pekee dhidi ya Southampton (15) na West Ham (11) ndiye aliyechangia mabao mengi zaidi kwa Spurs.

Guardiola ameshindwa mara mbili na Tottenham msimu huu, na amepoteza mechi nyingi za Chelsea tu (nane) kuliko Spurs (sita) katika maisha yake yote ya ukocha.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
NAMUNGO
VERSUS
MBEYA CITY
1 | 2.75
X | 2.60
2 | 2.84

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOURINHO ALIMWA NYEKUNDU, 'AGEUKA BUBU'




**ROME, Italia**

JOSE Mourinho alitolewa nje kwa kadi nyekundu baada ya kuubutua mpira kuelekea jukwaa la mashabiki wakati timu yake ya AS Roma ikilazimishwa sare ya mabao 2-2 na Hellas Verona kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Jumamosi.

'Giallorossi' hao, ambao hawakuwa na wachezaji muhimu kwa sababu ya majeraha na maambukizo ya mlipuko wa COVID-19, walipambana kutoka nyuma wakiwa wamelala 2-0 kwa mabao ya vijana Cristiano Volpato na Edoardo Bove walitokea benchi kuwarudisha mchezoni.

Lakini Mourinho hakuridhika, kutokana maamuzi ya mwamuzi, Luca Pairetto na mara kadhaa alijikuta akionywa.

Mourinho na Pairetto walikuwa wamezozana mara nyingi wakati wa mchezo huo, na matokeo ya mwisho yalikuwa pale Mreno huyo alipopiga mpira kwenye umati wa mashabiki katika Uwanja wa Olimpico na kujikuta akilimwa kadi nyekundu.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea, Tottenham, Manchester United na Inter alikataa kuzungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo na badala yake akaandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii.

"Ninawapenda watu hawa na kwa ajili yao, napigana," Mourinho aliandika kwenye Instagram.

"Siongei ni bora nirudi nyumbani nikale chakula cha jioni kizuri. Muwe na Jumapili njema."

# Anceloti: Madrid dhaifu kipindi cha kwanza

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti alikiri kwamba, uchezaji wa Real Madrid kipindi cha kwanza umekuwa "dhaifu" baada ya kuhitaji mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Marco Asensio, Vinicius Junior na Karim Benzema ili kupata ushindi wa 3-0 dhidi ya Alaves, Jumamosi.

Real Madrid iliingia kwenye mchezo huo ikitoka kufungwa bao 1-0 kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katikati ya wiki na Paris Saint-Germain.

Madrid ilionekana kutokuwa kwenye kiwango kizuri kipindi cha kwanza pale kwenye dimba la Bernabeu, kabla ya Asensio kufunga bao kwa shuti kali dakika ya 63.

Mshambuliaji huyo alicheza vizuri



na Karim Benzema na kumpa Vinicius bao la pili zikiwa zimesalia dakika 10, kabla ya Benzema kufunga mkwaju wa penalti katika muda wa nyongeza.

Matokeo hayo yameifanya Real Madrid kuwa mbele kwa pointi saba kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, huku Sevilla inayoshika nafasi ya pili ikicheza jana Jumapili.

"Tumezungumza kuhusu hilo wiki hii, ukweli kwamba ni ngumu kwetu kupata mabao kipindi cha kwanza," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi hiyo.

"Ni udhaifu ambao tumekuwa nao, na tutegemee tutaurekebisha."

Aliongeza: "Tulikuwa na dhamira, lakini tulikosa ubora katika nafasi ya tatu ya mwisho. Nilisema wakati wa mapumziko, ili kuongeza ubora zaidi, na wachezaji walifanya hivyo, zaidi ya washambuliaji wote watatu (Asensio, Vinicius na Benzema)."

Asensio mwenye umri wa miaka 26, sasa amefunga mabao saba ya ligi msimu huu, huku Benzema na Vinicius wakiwa na 18 na 13.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# UTOAJI NAMBA KILI MARATHON WAANZA KWA KISHINDO DAR

**Na Mwandishi Wetu**

MAMIA ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake wamejitokeza kwa wingi katika viwanja vya Mlimani City mwishoni mwa wiki kuchukua namba zao za kushiriki mbio maarufu za Kilimanjaro Premium Lager Marathon 2022.

Waandaaji wa mbio hizo wamesema mwitikio ulikuwa mkubwa kwani washiriki wengi walifika kwa muda na kufanya mchakato huo kwenda vizuri.

Meneja wa Bia ya Kilimanjaro Premium Lager, Irene Mutiganzi, akizungumza na mwandishi wetu mwishoni mwa wiki alisema zoezi hilo lilienda vizuri kwani washiriki walipata namba bila kusubiri muda mrefu.

Alisema wengi waliochukua namba ni washiriki wa mbio za Kilimanjaro Premium Lager Km. 42 na Tigo Km. 21 huku pia wa kilometa tano wakijitokeza na wengine wakiendelea kujisajili.

"Usajili kwa ajili ya mbio za Km. 42 na 21 tayari umefungwa, lakini bado tunauza namba za kilometa tano. Kwa ujumla zoezi lilikuwa limepangiliwa vizuri kwani tumeshuhudia washiriki wakiingia na kuondoka kwa haraka," alisema huku akitoa wito kwa wakazi wa Arusha wajitokeze kwa wingi kwenye ugawaji wa namba utakaoanza kesho, Jumanne.

Zoezi hilo litafanyika katika Hoteli ya Kibo Palace kesho, Jumanne na Jumatano kuanzia saa nane kamili hadi saa moja kwa siku hizo mbili kwa Arusha kabla ya kumalizikia Moshi ambapo namba hizo zitatolewa katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Alhamisi hadi kuanzia saa sita mchana hadi saa 12:00 jioni kabla ya kuhitimishwa Jumamosi saa 11:00 jioni.

"Washiriki waliojisajili wanatakiwa kuzingatia muda wa zoezi hili katika vituo husika ili kuepusha usumbufu na zoezi likishafungwa hakutakuwa na ugawaji wa namba siku ya mashindano," walisema waandaaji hao.

Waliongeza kuwa usajili kwa ajili ya mbio za kilomita tano bado unaendelea kwa njia ya Tigo Pesa kwa kubonyeza *149*20# na pia utafanyika katika vituo vya kutolea namba.

Wadhamini wa mbio za Kilimanjaro Marathon 2022 ni Kilimanjaro Premium Lager (Mdhamini Mkuu) Tigo (Km. 21 na Grand Malt (Km. 5).

Wadhamini wa meza za maji ni pamoja na Absa Tanzania, Unilever Tanzania, TPC Sugar, Simba Cement na Kilimanjaro Water. Wasambazaji rasmi ni GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel, CMC Automobiles na Surveyed Plots Company Ltd (SPC) na Bodi ya Utalii (TTB).




Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam waliojitokeza katika viwanja vya Mlimani City mwishoni mwa wiki kuchukua namba zao za kushiriki mbio maarufu za Kilimanjaro Premium Lager Marathon 2022. **MPIGAPICHA WETU**

# Simba Queens mechi 11, mabao 58, Opah tishio

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya soka ya wanawake ya Simba, Simba Queens, imeweka rekodi ya aina yake kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, baada ya kumaliza mzunguko wa kwanza kwa kushinda mechi zote 11 ilizocheza, huku straika wake hatari Opah Clement peke yake akipachika mabao 19 mpaka sasa.

Hii ina maana kuwa timu hiyo imezifunga timu zote zinazoshiriki ligi hiyo, ikiwa ni rekodi ambayo haijawahi kuwekwa na timu yoyote tangu kuanzishwa kwa Ligi Kuu hiyo.

Wiki iliyopita Simba Queens ilimaliza mzunguko wa kwanza kwenye Uwanja wa Mo Arena, ikiiangamiza Fountain Gate Princess kwa mabao 3-1, hiyo ikiwa ni mechi ya kwanza kwa wageni hao kupoteza katika ligi hiyo.

Haikuwa mechi rahisi, kwani muda mrefu timu hizo zilikuwa zikitoka sare ya bao 1-1, huku Simba Queens, ikipata mabao mawili ya haraka haraka mwishoni mwa mchezo.

Ni ushindi ambao umeiwezesha timu hiyo kufikisha mabao 58, huku ikiwa imevuna pointi 33 kwenye mechi zote ilizocheza za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake ambayo inajumuisha timu 12.

Timu zote 11 zilizokutana na zahama ya Simba ni Baobab Queens, The Tigers, Queens, Alliance Queens, JKT Queens, Fountain Gate Princess, Mlandizi Queens, Ruvuma Queens, Oysterbay Girls, Yanga Princess na TSC Queens.

Kwenye mechi hiyo Opah, alipewa tuzo na pesa taslim kiasi cha Sh. 500,000, kutokana na kuwa mchezaji bora wa mwezi Januari.

Wakati huo huo, Yanga Princess ilichapa Ruvuma Queens mabao 3-0, na kupanda hadi nafasi ya sita kwa pointi 14.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 21/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3671 | SP. Braga U23 vs Leixoes SC U23 | 1.80 | 3.28 | 4.15 |
| 14:00 | 5111 | Pars Jonoubi Jam vs Mes Shahr-e Babak | 2.60 | 2.60 | 3.45 |
| 14:00 | 5721 | Esteghlal Khuzestan vs Saipa Karadj | 2.24 | 2.80 | 3.85 |
| 14:30 | 2251 | Manisa BBSK vs Umraniyespor | 2.41 | 3.24 | 2.66 |
| 15:35 | 1877 | AL Adalh vs AL Ain | 2.09 | 3.04 | 3.42 |
| 16:00 | 1353 | Ipswich U23 vs Watford U23 | 1.32 | 5.21 | 6.57 |
| 16:00 | 1720 | Sheffield Wednesday U23 vs Crewe U23 | 1.60 | 4.06 | 4.35 |
| 16:00 | 3787 | Namungo vs Mbeya City | 2.75 | 2.60 | 2.84 |
| 16:00 | 3984 | APR FC vs Etincelles | 1.19 | 5.60 | 12.55 |
| 16:00 | 4104 | Sebeta City FC vs Bahir Dar Kenema FC | 2.99 | 2.79 | 2.46 |
| 16:00 | 4110 | Musanze vs Etoile de Lest | 1.82 | 3.28 | 4.05 |
| 16:00 | 4910 | Bugesera FC vs Rayon Sports FC | 3.08 | 2.89 | 2.33 |
| 16:15 | 1492 | Bisha FC vs AL Jeel | 2.70 | 2.84 | 2.65 |
| 16:15 | 3427 | Al Orubah vs Najran SC | 2.22 | 2.84 | 3.37 |
| 16:30 | 2271 | US Lecce youth vs Hellas Verona Youth | 1.89 | 3.52 | 3.48 |
| 16:30 | 3052 | Persipura Jayapura vs Persepam MU | 3.80 | 3.23 | 1.90 |
| 16:45 | 1801 | Al Ahli Doha SC vs Al Sadd SC | 12.52 | 7.51 | 1.13 |
| 17:00 | 2278 | Metalac vs Vojvodina | 3.28 | 3.18 | 2.08 |
| 17:00 | 2410 | Bengaluru FC vs Delhi Dynamos FC | 1.69 | 3.95 | 3.95 |
| 17:00 | 2802 | Adanaspor vs Erzurum BB | 3.33 | 3.18 | 2.06 |
| 18:15 | 4981 | Al Khaleej Club vs AL Draih | 1.81 | 3.32 | 4.05 |
| 18:30 | 1493 | Arab Contractors vs Smouha Club | 3.20 | 3.11 | 2.27 |
| 18:30 | 2307 | Farul Constanta vs Argesul Pitesti | 1.89 | 3.24 | 4.12 |
| 18:30 | 4777 | Inter Youth vs Bologna Youth | 1.32 | 4.99 | 6.91 |
| 18:55 | 2444 | Qatar SC vs Lekhwiya SC | 5.39 | 4.24 | 1.47 |
| 19:00 | 2426 | Ethiopia Bunna SC vs Fasil Kenema | 3.75 | 3.00 | 2.16 |
| 19:00 | 3962 | Radnik Surduluca vs FK Napredak | 2.31 | 3.07 | 2.93 |
| 19:30 | 1428 | NK Radomlje vs Maribor | 3.94 | 3.60 | 1.76 |
| 20:00 | 2499 | Goeztepe vs Galatasaray | 2.87 | 3.26 | 2.38 |
| 20:00 | 2989 | Altinordu vs Bandirmaspor | 3.81 | 3.62 | 1.78 |
| 20:00 | 3568 | Eyupspor vs Menemen Bld | 1.26 | 5.19 | 8.84 |
| 20:00 | 4011 | Wisla Krakow vs Gornik Leczna | 1.68 | 3.57 | 4.44 |
| 21:00 | 1382 | 1860 Munich vs Hallescher | 1.75 | 3.65 | 4.24 |
| 21:00 | 3272 | Randers vs Viborg FF | 1.84 | 3.50 | 4.04 |
| 21:00 | 5669 | Benfica Lisbon B vs Sporting Farense | 2.11 | 3.32 | 3.22 |
| 21:00 | 5871 | Talaea El Gaish vs Farco FC | 2.46 | 3.00 | 3.00 |
| 21:00 | 5905 | Cagliari vs Napoli | 5.57 | 4.38 | 1.53 |
| 21:30 | 4681 | Maccabi Haifa vs Hapoel Tel Aviv | 1.22 | 5.41 | 10.63 |
| 22:00 | 3149 | CF Estrela vs Varzim | 1.85 | 3.32 | 4.10 |
| 22:00 | 3256 | Jong AZ Alkmaar vs NAC Breda | 3.03 | 3.37 | 2.19 |
| 22:00 | 3809 | Jong Utrecht vs SBV Excelsior | 4.01 | 3.92 | 1.72 |
| 22:00 | 5277 | Jong Ajax vs Almere City | 1.67 | 4.01 | 4.21 |
| 22:45 | 3430 | Bradford PA vs Leamington | 2.64 | 3.36 | 2.36 |
| 22:45 | 4639 | Toulouse vs Le Havre | 1.62 | 3.58 | 5.49 |
| 22:45 | 5114 | Red Star vs Annecy FC | 2.64 | 2.83 | 2.83 |
| 23:00 | 3366 | Celta Vigo vs Levante | 1.62 | 4.01 | 5.22 |
| 23:00 | 3440 | Virtus Entella vs AC Siena | 1.91 | 3.36 | 4.05 |
| 23:00 | 3966 | Bologna vs Spezia | 1.80 | 3.69 | 4.29 |
| 23:00 | 4962 | Amorebieta vs Leganes | 2.89 | 2.99 | 2.50 |
| 23:15 | 5100 | Santa Clara vs Portimonense | 2.07 | 3.20 | 3.59 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Februari 21, 2022

Nipashe


UKURASA 22




## Mourinho alimwa nyekundu, 'ageuka bubu'

UPO VIZURI...



Beki wa Yanga, Shabani Djuma, akimjaribu mlinda mlango wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa na mechi dhidi ya Mtibwa Sugar itakayopigwa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, Jumatano. **PICHA: YANGA**

## Neymar na rekodi zaidi ya Messi, CR7


**LONDON, England**

HAKUNA shaka kwamba, Ronaldo Nazario de Lima ni mmoja wa wachezaji wakubwa zaidi ambao Brazil wamewahi kuwa nao. Alipata mafanikio mengi katika maisha yake ya soka, hata katika umri mdogo sana. Lakini Ronaldo alikuwa mzuri kiasi gani akiwa na umri wa miaka 21 na analinganaje na mastaa wanaochipukia wa siku hizi? **UK. 11**

## Nyota 10 waliotupia penalti nyingi zaidi

**LONDON, Uingereza**

KARNE ya 21 imekuwa na mapinduzi katika soka kwa njia zaidi ya moja. Mtindo wa soka umebadilika msimu baada ya msimu na kasi yake inakuwa bora kadri muda unavyopita.



**UK. 12**

# NABI AIHOFIA YANGA SC KWA MTIBWA MANUNGU

●●●Kujichimbia Morogoro leo na nyota 25 kujiandaa kwa mechi hiyo ya Jumatano, asema...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI kikosi chake kikitarajia kuondoka leo jijini Dar es Salaam kuelekea mjini Morogoro kujiandaa kwa siku moja kabla ya Jumatano kwenda Manungu, Turiani kuivaa Mtibwa Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema wataingia katika mechi hiyo kwa tahadhari kubwa na wanautazama mchezo huo kama fainali.

Yanga itashuka katika Uwanja wa Manungu Complex ulioko Turiani takriban kilometa 85 kutoka mji wa Morogoro kuivaa Mtibwa Sugar ambayo iliikomalia Simba uwanjani hapo na kupata sare tasa katika mechi ya Ligi Kuu msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema wataingia katika mchezo huo kama fainali kutokana na ushindani mkubwa ulioko Ligi Kuu kwa sasa, lakini rekodi ya wapinzani wao katika michezo iliyopita wakicheza uwanjani hapo.

Alisema wamefanya maandalizi mazuri na kuna mambo wameendelea kupambana nayo ikiwamo stamina pia kuhakikisha wanakuwa na ubora mkubwa na washambuliaji kutumia nafasi wanazotengeneza.

"Tunawaheshimu sana wapinzani wetu, kwetu kila mechi imekuwa fainali, kwa sababu hatujawahi kuwa na mchezo rahisi," alisema na aliongeza;

"Nimewaona wapinzani wetu (Mtibwa Sugar), na rekodi haziko vizuri tunapokutana nao, tutacheza kwa tahadhari kubwa ili kupata matokeo chanya na pointi tatu katika mchezo huu," alisema Nabi.

Alisema ingawa wana idadi kubwa ya wachezaji majeruhi lakini wapo wengine wanaoweza kupambania timu na kupata matoke mazuri dhidi ya Mtibwa Sugar.

Kuhusu uwanja, Nabi alisema wamefanyia kazi na anatumai kupata matokeo mazuri katika mchezo huo ambao wanahitaji pointi tatu ili kuendelea kujiimarisha kileleni.

"Tusiwe na hofu juu ya uwanja kwa sababu kila kitu kimeenda vizuri ukizingatia mechi yetu dhidi ya Mbeya City tulicheza uwanja mzuri wa nyumbani na kuondoka na pointi moja," alisema Nabi.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, ambaye tayari yupo mkoani Morogoro akiendelea na zoezi la uandikishaji wa wanachama, alisema kwa mujibu wa kocha hali za wachezaji zinaendelea vizuri na kwamba kikosi kitaondoka na wachezaji 25.

"Kikosi chetu kinaendelea vizuri kesho (leo) timu yetu itaondoka jijini Dar es Salaam mapema kwa sababu wachezaji wanatakiwa wawahi kufika mapema waanze mazoezi hapa," alisema Bumbuli.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >